# القرآن الحكيم

# QURANI TAKATIFU

Swahili Quran Translation

Juzuu - ONE (Alif Lam Mym)

by
Sheikh Abdullah Saleh Al-Farsy

بسم الله الرحمن الرحيم

# SURATUL FATIHA*

Imeitwa kwa jina tukufu hili kwa ajili ya mnasaba wake na muwafaka wake kwani tamko la "Fatiha" katika Kiarabu maana yake ni *chanzo* (mwanzo) cha kila kitu kile — kikiwa maneno au kitendo. Basi hii *Suratul Fatiha* ndiyo dibaji na ndio utangulizi wa Qurani.

*Wakati wa Kuteremka Kwake:*

Imeteremka Sura hii mwanzo wa kuja Utume. Na hii ndiyo Sura ya awali kuteremka kamili. Kabla yake ziliteremka Aya Aya tu zilizomo katika Sura ya Iqraa na *Suratul Muddaththir* na *Suratul Muzzammil.*

*Yaliyo Ndani Yake:*

Hii ni dua Mwenyezi Mungu anamwamrisha kuomba kila anayeanza kujifundisha kukijua kitabu chake. Muradi Wake ajikurubishe mtu kwa Mwenyezi Mungu kwa dua hii kabla ya kukianza kukisoma hiki kitabu chake; ikiwa kweli anataka kupata faida ndani yake.

Na ni tabia ya Binadamu kuwa haombi ila kile kinachotakiwa na moyo wake; wala hamwombi ila yule ambaye ana hakika kuwa kitu hicho kiko mikononi mwake. Imekuwa hapa Mwenyezi Mungu anamfundisha mwanaadamu — kwa dua hii anayoisoma mwanzo wa kitabu chake — kuwa akikisoma kitabu hiki akisome kwa nia ya kutaka aongozwe njia iliyonyoka, aongolewe vizuri aongoke. Na ajue kuwa msingi wa kujulia atakayoyajua ni Mwenyezi Mungu. Basi aanze kusoma kitabu hiki kwa kumwomba Mwenyezi Mungu Uongofu na Hidaya.

Ukifahamu haya utaona kuwa hii *Suratul Fatiha* si utangulizi khasa wala dibaji ya Qurani, kama zile dibaji za vitabu vyengine. Lakini baina yake hii Fatiha na Qurani yote nzima ni kama dua na jawabu. Hii Fatiha ni dua inayotokana na mja kumwomba Mola wake, na Qurani nzima ni Jawabu ya Mola kumjibu mja Wake. Yeye kamwambia Mwenyezi Mungu "Niongowe"; na Mwenyezi Mungu kamwambia "Huu Uwongofu wako, ufuate." Basi natufuate kila kilichomo ndani ya hii Qurani ili tuwe tumekwisha kuongoka kama tulivyoomba tuongolewe.

---

Qurani tukufu, kwa ajili ya kusahilishwa, imegawanywa mafungu thalathini, ambayo karibu yanafanana urefu wake. Kila fungu huitwa "Juzuu". Katika Qurani ziko Sura 114, kila Sura ilipewa jina na kuwekwa mahali ilipo na mwenyewe Mtume s.a.w. Sura ni fungu la maneno lenye mwanzo na mwisho. Sura ziko kubwa na ndogo. Na uchache wa iliyo ndogo kabisa ni kukusanya Aya tatu. Jina la Sura ghalibu hufuwata kitu au jambo lililotajwa ndani yake: kama *Suratul-Baqarah* (Sura ya Ng'ombe); imeitwa kwa jina hili kwa sababu ya kutajwa kisa cha ng'ombe wa Bani Israil ndani yake.

Sura hii ina majina mengi, zaidi inajulikana kwa jina la *Fatihatul - Kitab* (Mwanzo wa Kitabu — yaani Qurani). Na huitwa pia *Suratus - Salaat* (Sura ya Kusalia), *Assab'ul - Mathani* (Aya saba zinazosomwa mara kwa mara katika Sala), *Ummul-Quran* (Asli ya Qurani au Msingi wa Qurani). Na imeitwa kwa jina hili kwa sababu imekusanya kwa ufupi Muradi wa Qurani nzima. Qurani imekusanya mambo matano: (a) *Tawhid,* yaani kuamini kuwa Mwenyezi Mungu ni Mmoja, na Ndiye Peke Yake wa kuabudiwa; (b) Kufundisha watu namna ya kumwabudu Mwenyezi Mungu; (c) Kuwaongoza watu katika njia itakayowafikisha kwenye wema wa duniani na Akhera; (d) Kuwafunulia watu malipo mema kwa wanaofanya mema, na malipo mabaya kwa wanaofanya mabaya; na (e) Kuwapa habari za watu waliotangulia, ambao walishikamana na mambo mema waliyoamrishwa na Mwenyezi Mungu, na habari za waliokhalifu amri Zake wakafanya maovu, na mwisho wa kila mmoja katika makundi mawili hayo, ili watu wapate kuzingatia waache mabaya na wafanye mazuri. Yote haya yamo katika Sura hii, pamoja na ufupi wake. Kwa hivyo Sura hii imekuwa tukufu sana, ndiyo ikafanywa ni Sura ya kusalia ambayo hapana Sura nyengine inayoweza kuwa badili yake, kama utakavyoona.

اٰيَاتُهَا (١) سُوْرَةُ الْفَاتِحَةِ مَكِّيَّةٌ (٥) رُكُوْعُهَا ١

*Ina Aya 7*

## SURATUL FATIHA

*(Imeteremka Makka)*

1. Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ (١)

2. Shukrani zote anastahiki Mwenyezi Mungu, Mola wa walimwengu wote

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ رَبِّ الْعٰلَمِيْنَ (٢)

3. Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo

الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ (٣)

4. Mwenye kumiliki siku ya malipo.

مٰلِكِ يَوْمِ الدِّيْنِ (٤)

5. Wewe tu ndiye tunayekuabudu, na wewe tu ndiye tunayekuomba msaada.

اِيَّاكَ نَعْبُدُ وَاِيَّاكَ نَسْتَعِيْنُ (٥)

6. Tuongoze njia iliyonyoka

اِهْدِنَا الصِّرَاطَ الْمُسْتَقِيْمَ (٦)

7. Njia ya wale uliowaneemesha; siyo (ya wale) waliokasirikiwa, wala (ya) wale waliopotea.

صِرَاطَ الَّذِيْنَ اَنْعَمْتَ عَلَيْهِمْ ۙ غَيْرِ الْمَغْضُوْبِ عَلَيْهِمْ وَلَا الضَّآلِّيْنَ (٧)

---

1. Katika kuanza kila jambo jema inatakiwa katika dini ya Kiislamu kulianza kwa kupiga ***Bismillahi.*** Kwa hivyo kila sura imeanzwa kwa ***Bismillahi ila Suratit Tawba;*** kwa kuwa Masahaba wengine walisema kuwa hiyo na ***Suratil Anfal*** ni sura moja—hiyo ***(Anfal)*** ni kipande cha kwanza na ***at Tawba*** ni kipande cha pili.

Tamko hili "kwa" tumefasiria harufu "Ba" iliyoanzia ***Bismillah.*** Harufu hii kwa Kiarabu itakapoingia katika jina la mtu au kitu huonyesha kutaka msaada kwa mtu yule au kitu kile katika kitendo unachofanya. Hapa maana yake yatakuwa haya "Ninasoma pamoja na kutaka msaada kwa Jina la Mwenyezi Mungu."

Tamko ***Allah*** halitumiki ila kuwa ni Jina la Mwenye Kuumba kama vile linavyotumika tamko "Mwenyezi Mungu" kwa Kiswahili. Kwa hivyo "Mwenyezi Mungu" ndiyo tafsiri ya sawa ya ***Allah.*** Ni makosa kufasiri ***Allah*** kwa "Mungu", sababu tamko hili wakati mwengine linatumiwa kwa asiyekuwa Mungu wa haki Mwenye kuumba. Na pia tamko "mungu" lina jam'u ***(plural),*** husemwa "mungu" na "miungu". Tamko "Mwenyezi Mungu" halina ***plural*** vile vile kama tamko ***Allah.***

2. Aya hii inaonyesha kuwa wa kushukuriwa kweli kweli ni Mwenyezi Mungu, kwani Yeye ndiye aliyetuumba sisi na kila kiumbe. Na kila neema tuliyo nayo — kubwa na ndogo — imetufika kwa kutaka Yeye. Lau kuwa hataki zisingetufika. Na hao ambao zimetufika neema hizo kwa sababu zao, hao ni sababu tu alizojaalia Mwenyezi Mungu zitufike neema hizo kwa sababu zao. Lakini mtoaji hakika ni Yeye Mwenyewe. Lakini juu ya hivyo hao walio sababu inataka nao washukuriwe. Akisema Mtume kuwa "Asiyewashukuru viumbe (nao), basi hatakuwa kamshukuru Mwenyezi Mungu." Basi daima tuzikumbuke na tuzishukuru ihsani tulizofanyiwa na tuwashukuru hao waliotufanyia.

Tamko hili "Rabbi" hufasiriwa "Mola" au "Bwana"; na yote ni maana mamoja, kwani tamko "Mola" asili yake ni tamko la Kiarabu ***Mawla*** ambalo maana yake ni "Bwana." Lakini tamko ***Rabbi*** lina maana ya ulezi ndani yake. Yaani baada ya kuwa Yeye ni Bwana wa viumbe, vile vile Ndiye Mwenye kuwalea kwa kuwafundisha na kuwatendea kila litakalowafaa katika dunia yao na Akhera yao. Hapana Bwana mwengine anayeweza kufanya kama hayo. Na hili latufundisha ***Tawhid,*** yaani kumwabudu Mwenyezi Mungu Mmoja Peke Yake, ambalo ndilo jambo kubwa katika Dini na sababu kubwa ya kuletwa Mitume na Kuteremshwa vitabu.

4. Hapa pana misomo miwili *Maaliki* (mwenye kumiliki), na *Maliki* (yaani mfalme). Kwa zote njia mbili, Aya hii inatufundisha kuwa kuna siku ya malipo ambayo mtu atalipwa kwa aliyoyafanya hapa ulimwenguni ikiwa mazuri au mabaya. Na makusudio ya kupewa habari hii ni kutakikana tuache mabaya na tufanye yaliyo mazuri.

5. Aya hii inaonyesha kuwa hapana ruhusa kuabudiwa ila Mwenyezi Mungu, wala hapana ruhusa kuombwa msaada kwa waliokufa wala mizimu wala mapango wala mengineyo. Wala kuwawekea manadhiri. Haramu kabisa mambo hayo. Wa kuombwa na kuwekewa manadhiri ni Mwenyewe tu Mwenyezi Mungu peke yake. Hata wazee wanawake wa zamani kabla ya mambo kuharibiwa wakiimba:-

Mwambie mama aombe: na miye niombe
Muombwa ni Yeye Rabbaana.

7. Aya hii inaonyesha kuwa waliopotea wanagawanyika sehemu mbili—ima wamepotea kwa kuwa hawajui: *Adhdhaallyn*. Au wanajua lakini hawafuati: *Al Maghdhubi Alayhim*. Na hawa ndio wabaya zaidi.

Sehemu zote mbili hizi zinahisabika kuwa zimepotea. Wala ujinga hauwi udhuru, kwani ni wajibu wa kila mtu kujifundisha kiasi cha kujua kuwa hili linafaa na hili halifai ili ajiepushe na lisilofaa na afanye linalofaa.

Na maadamu pana neno la Mwenyezi Mungu au Mtume Wake, basi halifuatwi neno la mtu mwengine. Ikiwa si hivyo mtu huyo atakuwa kapotea upotevu ulio dhahiri, kama alivyosema Mwenyezi Mungu.

. Katika Aya ya 7 *An-amta Alayhim* kuna watu (Makadiyani) wanaodai kuwa Aya hii imewafiki Aya ya 69 ya Sura ya 4 (yaani *Suratun Nisaa, Walmuhsanat)* na imewafiki Aya ya 20 ya sura ya 5 yaani *Suratul Maida, Laa Yuhibbu)* na wakasema ". . . neema hizo zimesemwa kuwa ni Unabii na ufalme. Aya hii inadhihirisha ya kuwa neema hizo zote zitaendelea kupatikana. Manabii wataendelea kufika . . ."

Tazama uwongo wao huo! Wapi katika Aya hizi 3 panapoonyesha kuwa Utume utaendelea? Tuchukue hata tafsiri yao tutazame walivyofasiri hiyo Aya ya 7 ya *Suratul Fatiha*. Wameifasiri hivi: "Njia ya wale uliowaneemesha." Na hiyo Aya ya 20 ya Sura ya 5 *Suratul Maida* wameifasiri: "Na (kumbukeni) Musa alipowaambia watu wake: Enyi watu wangu! Kumbukeni neema za Mwenyezi Mungu zilizo juu yenu, Alipowafanya manabii kati yenu na Akawafanyeni wafalme, na Akawapeni ambayo Hakuwapa wowote katika walimwengu."

Iko wapi humu kuwa Utume utaendelea baada ya Nabii Muhammad? Si makusudi hawa wanapoteza watu na kumsingizia Mwenyezi Mungu asiyoyasema? Na tutaona vile vile namna wanavyomsingizia Mtume na wanavyuoni wasiyoyasema. Khatari kabisa watu hawa. Wanasingizia — wakayatajia na vitabu — yasiyosemwa. Hawamwogopi Mwenyezi Mungu hata chembe.

Ama Aya ya 69 ya Sura ya 4 *(Suratun Nisaa)* hiyo wameipoteza mpaka tafsiri yake, siyo wameisambukizia yasiyokuwamo tu. Wamelichukua tamko la Kiarabu la *Ma'a* (ambalo maana yake "Pamoja" kama anavyojua kila aliyesoma Kiarabu), wakalifanya kuwa tamko la Min (miongoni); wakafasiri hivi "Na mwenye kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume, basi hao ni *miongoni* mwa wale Aliowaneemesha Mwenyezi Mungu — Manabii . . ." Na hali ya kuwa tafsiri yake sahihi ni "Na wenye kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume, basi hao *watakuwa* pamoja na Manabii. . ." Hata wao wanajua kwa yakini kuwa hii ndiyo tafsiri sahihi ya Aya hii, lakini wameipindua kusudi ili wapoteze Waislamu, wawe makafiri. Ndio raha yao.

Kisha wakamsingizia Marehemu Sheikh Al Amin bin Ali Mazrui kuwa kakubalisha kuwa Utume utaendelea baada ya Nabii Muhammad wakasema: "Sheikh Al Amin bin Aly ameandika katika tafsiri yake ya Juzuu ya *Alif Lam Mym,* ukurasa wa 4, maelezo ya Aya hii kama hivi: "Aya mbili hizi zatupa khabari ya watu waliotangulia kabla yetu na katika watu hao kuna ambao walikuwa wameshikamana na mambo mema, ambayo yatupasa nasi kushikamana nayo tupate ongoka kama walivyoongoka hao, na watu hao ni Mitume. . ."

Iko wapi hapa kuwa Sheikh Al Amin kasema kuwa utaendelea Utume baada ya Nabii Muhammad? Si makusudi tu hawa wanawasingizia uwongo wanavyuoni ili wapoteze Waislamu? Na tutahadhari na maadui hawa wa Uislamu. Kasema Sheikh Al Amin "tupate ongoka kama walivyoongoka hao. . ."

Na hivi ndivyo Mwenyezi Mungu alivyomwambia Mtume na Masahaba — kama ilivyo katika Aya ya 112 ya *Suratu Hud*—"Endelea na uwongofu kama ulivyoamrishwa; (wewe) na wale wanaoelekea (kwa Mungu) pamoja nawe. . ." Basi hao waliokuwa pamoja na yeye (Masahaba) walikuwa Mitume? Si makusudi tu wanawapoteza Waislamu? Maadui kweli kweli hawa wa Uislamu.

Khalafu katika sahifa 162 ya tafsiri yao katika kufasiri hiyo Aya ya 69 ya *Suratun Nisaa* wameipotoa vile vile tafsiri ya Ma'a, wakasema maana yake "miongoni" siyo "pamoja". Lakini Mwenyezi Mungu kawahizi. Wenyewe walipoifasiri Aya ya 146 ya hii hii Sura 4 katika sahifa 181 waliifasiri ". . . basi hao wako pamoja na waaminio . . ."

Na katika sahifa hiyo hiyo 162 wakaipindua tafsiri ya *Ma'a* (pamoja) iliyoko katika Aya ya 193 ya Sura ya 3 *(Aali Imran)*. Lakini Mwenyezi Mungu kawahizi tena. Walipoifasiri katika sahifa 140 waliifasiri hivi ". . . Utufishe pamoja na watu wema".

Na katika hiyo sahifa 162 wamesema kuwa mwenye *Ruhul Maany* . . . ameandika: "Unabii ni wa namna

mbili, *wa desturi* na *wa maalumu*. Unabii *wa maalumu* yaani Utume wa kuleta Sheria, sasa haupatikani; lakini utume *wa desturi* bado unaendelea. . ."

Tazama khiana ya Makadiani. Wallahi hamna humo katika *Ruhul Maany* katika kufasiri Aya hii katika sahifa 69 juzuu ya 4 neno la Unabii "wa desturi na wa maalumu" au kuwa kakubalisha huyo mfasiri mkubwa kuwa inamjuzia mtu kujita Mtume (Utume wa desturi).

Wallahi! Uwongo. Na ukafiri mkubwa kabisa huu wa kumsingizia Mwenyezi Mungu na Mtume na wanavyuoni wasiyoyasema ili wawapoteze Waislamu. Asiyepekua kwa jicho lake akaona uwongo kabisa wa "quotations" zao asingesadiki kuwa binadamu hufikilia daraja hii ya kusingizia vitabu yasiyokuwamo humo. Nadhani kazi hii chafu kabisa wanaifanya hawa Makadiyani peke yao. Wanasema uwongo ulio dhahiri kabisa. Na wanataja matabu makubwa kabisa yenye majuzuu (volumes) mengi ambavyo wana yakini kuwa watu wengi kabisa hawana vitabu hivyo, kama hii *Ruhul Maany* majuzuu 20 na hiyo *Bahrul Muhyt* yenye majuzuu kama haya. Lakini *Alhamdulil Lah* — tunavyo.

Basi huyu mwenye *Ruhul Maany* katika kufasiri Aya hii ya *Suratun Nisaa* katika kuifasiri Aya hii waliyoisema kuwa ni Aya ya 70, aliandika humo dhahiri shahiri kuwa hakuna ruhusa kudai Utume baada ya Nabii Muhammad. Alisema hapa katika Juzuu ya 4 ya tafsiri yake katika sahifa 69.

Alisema katika mstari wa 17 "Mlango wa kutumia tamko la Utume (yaani baada ya Nabii Muhammad) umefungwa". Akasema katika mstari wa 19: "Imezuilika juu yetu kutumia tamko la Utume" (baada ya Nabii Muhammad). Na akasema katika mstari wa 26: "Na mwenye kupindukia daraja ya *Siddiiqina* anaingia kwenye Utume. Na huo ni mlango uliofungwa"

Mnaona Makadiyani walivyomsingizia uwongo huyu mfasiri kuwa anakubali kuwa Utume unaendelea.

Na katika hiyo hiyo sahifa 162 wakasingizia kuwa mwenye *Bahril Muhyt* amenakili maneno ya *Raghib* kuwa kasema: "Mwenyezi Mungu *amewagawanya* waaminio katika sehemu nne katika Aya hii na amewawekea madaraja mane ambayo mengine yao ni ya chini kuliko mengine na amewahimiza waaminio wasibakie nyuma ya madaraja haya".

Uwongo! Hakusema hiki kipande cha mwisho kinachosema "na amewahimiza waaminio wasikae nyuma ya madaraja haya".

Maneno haya ya Ar Raghib hata mwenye *Ruhul Maany* ameyataja katika sahifa 69 mstari wa 4, pasi ya kuwapo kipande hicho walichokipachika Makadiyani kuwa "na amehimiza waaminio wasikae nyuma ya madaraja haya".

Waongo wazandiqi Makadiyani. Hawajali hata chembe kusema uwongo. Na maadamu tumekwisha kuwajua kuwa waongo natusiwasadiki kwa lolote lile tusilolijua — wanalolisema. Wamezua — na wanazua — haya na mengine tena. Waimbiwe: *Akalikwakwara kwaka.*

Na katika sahifa 163 wakaitaja Hadithi iliyopokewa na Ibn Maajah kuwa Mtume kasema: "Kama (mwanangu) Ibrahimu angeishi angekuwa Nabii." Na huyo mfasiri wao anajua kwa yakini kuwa Hadithi hii si sahihi na anajua kuwa papo hapo katika huu mlango wa jeneza imebainishwa kuwa Hadithi hii si sahihi. Na katika vitabu vyote vinavyotaja Hadithi imebainishwa kuwa Hadithi hii si sahihi. Anajua barabara haya, lakini anataka tu kupoteza Waislamu kama ada yao na raha yao. Ada yao na raha yao kutaka kuwapoteza Waislamu.

Tutahadhari na kuwasadiki na majidai yao ya kusema Kitabu fulani kinasema hivi, Kitabu fulani kinasema hivi. Huo uwongo kabisa. Havikusema kabisa vitabu hivyo. Au huwa wamemegua humo wasiyoyataka ili *yadhanishe* vyengine, kama walivyomegua hapa kutaja kuwa Hadithi hiyo imebainishwa humo humo kuwa si Hadithi sahihi. Au hugeuza maana khasa kama walivyogeuza maana ya Aya ya 70 ya Sura ya 4.

اٰيَاتُهَا ٢٨٦ (٢) سُوْرَةُ الْبَقَرَةِ مَدَنِيَّةٌ (٨٦) رُكُوْعَاتُهَا ٤٠

*Ina Aya 286* **SURAT AL - BAQARAH** *Ina Makara 40*

*(imeteremka Madina)*

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

الٓمّٓ ﴿١﴾

1. Alif Lam Mym.

ذٰلِكَ الْكِتٰبُ لَا رَيْبَ فِيْهِ هُدًى لِّلْمُتَّقِيْنَ ﴿٢﴾

2. Hiki ni Kitabu kisichokuwa na shaka ndani yake; ni uwongozi kwa wamchao Mwenyezi Mungu

الَّذِيْنَ يُؤْمِنُوْنَ بِالْغَيْبِ وَيُقِيْمُوْنَ الصَّلٰوةَ وَمِمَّا رَزَقْنٰهُمْ يُنْفِقُوْنَ ﴿٣﴾

3. Ambao huyaamini yasiyoonekana (maadam yamesemwa na Mwenyezi Mungu na Mtume wake) na husimamisha Sala na hutoa katika yale Tuliyowapa.

وَالَّذِيْنَ يُؤْمِنُوْنَ بِمَآ اُنْزِلَ اِلَيْكَ وَمَآ اُنْزِلَ مِنْ قَبْلِكَ وَبِالْاٰخِرَةِ هُمْ يُوْقِنُوْنَ ﴿٤﴾

4. Na ambao wanaamini yaliyoteremshwa kwako, na yaliyoteremshwa kabla yako na wanaamini (kuwa iko) Akhera.

---

1. *Alif Lam Mym.* Sura nyingi zinaanzwa kwa namna hii. Ili kuonyesha kuwa hii Qurani imefanywa kwa hizo harufu za *Alif Bee* mpaka *Yee*. Na kuambiwa makafiri: "Nyinyi mnasema kuwa 'Hii Qurani Kaizua Nabii Muhammad, hakuteremshiwa na Mwenyezi Mungu', basi hebu nyinyi fanyeni kama hii; harufu ndizo zizi hizi za *Alif Bee*." Basi hii ni moja ya sababu za kutajwa harufu hizi.

Na hili tamko la *Alif Lam Mym* tupu limetumiwa katika Sura 6: (1) Katika *Alif Lam Mym* ya *Suratul Baqarah* (iliyoteremka Madina) iliyo kwenye Juzuu ya *Alif Lam Mym;* (2) Katika *Alif Lam Mym* ya *Surat Aali Imran* (iliyoteremka Madina) iliyo kwenye Juzuu ya *Tilkar Rusul;* (3) Katika *Alif Lam Mym* ya *Suratul Ankabut* (iliyoteremka Makka) iliyo kwenye Juzuu ya *Amman Khalaq;* (4) Katika *Alif Lam Mym* ya *Suratur Rum* (iliyoteremka Makka) iliyo kwenye Juzuu ya Utlu; (5) Katika *Alif Lam Mym* ya *Surat Luqman* (iliyoteremka Makka) iliyo kwenye Juzuu ya *Utlu;* (6) Katika *Alif Lam Mym* ya *Suratus Sajda* (iliyoteremka Makka) iliyo kwenye Juzuu ya *Utlu.*

Na tamko la *Alif Lam Mym Raa* limetumika katika Sura moja iliyoteremka Madina, *Suratur Raad* iliyo katika Juzuu ya *Wamaa Ubarriu.*

Na tamko la *Alif Lam Mym Sad* limetumika katika Sura moja iliyoteremka Madina, *Suratul Aaraf* iliyo katika Juzuu ya *Walau Annanaa.*

Na limetumika tamko la *Alif Lam Raa* katika Sura 5: (1) Katika *Surat Yunus* iliyoteremka Makka iliyo kwenye Juzuu ya *Yaatadhirun;* (2) Katika *Surat Hud* iliyoteremka Makka iliyo kwenye Juzuu ya *Yaatadhirun;* (3) Katika *Surat Yusuf* iliyoteremka Makka iliyo kwenye Juzuu ya *Wamaa Min Daabbah;* (4) Katika *Surat Ibrahim* iliyoteremka Makka iliyo kwenye Juzuu ya *Wamaa Ubarriu;* (5) Katika *Suratul Hijr* iliyoteremka Makka iliyo kwenye Juzuu ya *Wamaa Ubarriu* na Rubamaa.

Na tamko la *Haa Mym* tupu limetumika katika Sura 6: (1) Katika *Suratul Muumin* iliyoteremka Makka iliyo kwenye Juzuu ya *Faman Adhlam;* (2) Katika *Surat Fussilat* iliyoteremka Makka iliyo kwenye Juzuu ya *Faman Adhlam;* (3) Katika *Suratuz Zukhruf* iliyoteremka Makka iliyo kwenye Juzuu ya *Ilayhi Yuraddu;* (4) Katika *Suratud Dukhan* iliyoteremka Makka iliyo kwenye Juzuu ya *Ilayhi Yuraddu;* (5) Katika *Suratul Jaathiya* iliyoteremka Makka iliyo kwenye Juzuu ya *Ilayhi Yuraddu;* (6) Katika *Suratul Ahqaaf* iliyoteremka Makka iliyo kwenye Juzuu ya *Haa Mym.*

Na tamko la *Haa Mym Ayn Syn Qaf* limetumika mara moja kwenye *Suratush Shuuraa* iliyoteremka Makka iliyo kwenye Juzuu ya *Ilayhi Yuraddu.*

Na tamko la *Sad* tupu limetumika mara moja kwenye *Surat Sad* iliyoteremka Makka iliyo kwenye Juzuu ya *Wamaa Liya.*

Na tamko la *Taasyn* limetumika mara moja kwenye *Suratun Naml* iliyoteremka Makka iliyo kwenye Juzuu ya *Waqalalladhyna*.

Na tamko la *Taasyn mym* limetumika katika Sura mbili: (1) Katika *Suratush Shuaraa* iliyoteremka Makka iliyo kwenye Juzuu ya *Waqalalladhyna;* (2) Katika *Suratul Qasas* iliyoteremka Makka kwenye Juzuu ya *Amman Khalaq*.

Na tamko la *Qaf* tupu limetumika mara moja katika *Surat Qaf* iliyoteremka Makka iliyo kwenye Juzuu ya *Haa Mym*.

Na tamko la *Kaf Haa Yaa Ayn Sad* limetumika mara moja katika *Surat Maryam* iliyoteremka Makka iliyo katika Juzuu ya *Qala Alam*.

Na tamko la *Nun* tupu limetumika mara moja kwenye *Suratul Qalam* iliyoteremka Makka iliyo kwenye Juzuu ya *Tabaarak*.

Na tamko la *Yaasyn* imetumika mara moja katika *Surat Yaasyn* iliyoteremka Makka iliyo kwenye Juzuu ya *Waman Yaqnut*.

4. Tamko la "na yaliyoteremshwa kabla yako" ni la kuonyesha kuwa Muislamu Hana ruhusa kuamini kuwa Mwenyezi Mungu atamteremshia Utume mtu mwengine BAADA ya Nabii Muhammad. Mtu akiwaamini hao waongo wanaosema kuwa wamepewa utume BAADA ya Nabii Muhammad, basi mtu huyo atakuwa kafiri tu.

Wameipotoa tafsiri ya Aya ya 5 (kwa mpango wao, na ya 4 kwa mpango wa dasturi). Wameipindua tafsiri ya tamko la *Wabil-Aakhirat*. Tafsiri yake khasa inayokubaliwa na wafasiri wote ni kuwa "Wanaiamini Akhera." Wao wamefasiri "wana yakini na yale yatakayokuja baadaye"

Wao Makadiani katika mwanzo wa tafsiri yao (VIII) wametaja chungu ya vitabu vya tafsiri ya Quran walivyovisoma hata wakafasiri hii tafsiri yao, kama wanavyojidai. Basi nawatazame humo, kama watamwona mmoja katika hao — na wengine — kafasiri hivi walivyofasiri wao, la katika Aya hii wala Aya nyingine zo zote zilizotaja tamko la "Al Aakhira" katika Quran. Tamko hili limetajwa katika Sura:

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | *Al Baqarah* | Mara 10 | 20. | *An Naml* | Mara 3 |
| 2. | *Aali Imran* | Mara 9 | 21. | *Al Qasas* | Mara 3 |
| 3. | *An Nisaa* | Mara 3 | 22. | *Al Ankabut* | Mara 3 |
| 4. | *Al Maida* | Mara 3 | 23. | *Ar Rum* | Mara 2 |
| 5. | *Al An—am* | Mara 3 | 24. | *Luqman* | Mara 1 |
| 6. | *Al Aaraf* | Mara 4 | 25. | *Al Ahzab* | Mara 2 |
| 7. | *Al Anfal* | Mara 1 | 26. | *Sabaa* | Mara 3 |
| 8. | *At Tawba* | Mara 4 | 27. | *Az Zumar* | Mara 3 |
| 9. | *Yunus* | Mara 1 | 28. | *Al Muumin* | Mara 2 |
| 10. | *Hud* | Mara 4 | 29. | *Fussilat* | Mara 3 |
| 11. | *Yusuf* | Mara 4 | 30. | *Ashshuuraa* | Mara 1 |
| 12. | *Ar Raad* | Mara 2 | 31. | *An Najm* | Mara 2 |
| 13. | *Ibrahim* | Mara 2 | 32. | *Al Hadid* | Mara 1 |
| 14. | *An Nahl* | Mara 7 | 33. | *Al Hashr* | Mara 1 |
| 15. | *Al Israa* | Mara 6 | 34. | *Al Mumtahina* | Mara 1 |
| 16. | *Taha* | Mara 1 | 35. | *Al Muddaththir* | Mara 1 |
| 17. | *Al Haj* | Mara 2 | 36. | *Al Qiyama* | Mara 1 |
| 18. | *Al Muuminun* | Mara 2 | 37. | *Al Layl* | Mara 1 |
| 19. | *An Nur* | Mara 3 | | | |

Hizi takriba ndizo mara zote ilipotajwa tamko la *"Al Aakhirat"*. Na mara zote hizo muradi wake ni siku ya Kiama, kama wafasiri wote walivyofasiri na kama ilivyo dhahiri ukitazama hata wewe mwenyewe. Na kama walivyofasiri wao pia — kwa kuwa Mwenyezi Mungu anataka kuwahizi wahizike. Na wamehizika. Hii moja tu ya mwanzo ndiyo wameipotezea tafsiri yake ili hizaya iwafike.

*Al Aakhirat* mbili tu — ya *Surat Sad* na *Suratun Naziat* — ndizo zilizoweza kufasiriwa kwa Akhera na Zinafasiriwa kwa jambo liliopita hivi karibuni; na *Al Aakhirat* ya mwanzo katika *Suratul Israa* inayofasiriwa kwa "wa mwisho." Lakini wao wamefasiri *Al Aakhirat* iliyoko mwanzo wa *Al Baqarah* kwa 'yatakayokuja baadaye;' yaani Utume wa baada ya Nabii Muhammad. Na tafsiri hii uwongo kabisa. Wakatia chini katika maelezo yake sahifa 7 mstari wa 32 "mcha Mungu ni yule anayeamini maneno yake yaliyoteremshwa katika kila zama na kila nchi. Yaani Waislamu wakubali kila ukweli uliopatikana kabla ya Uislamu, ukweli uliopo na utakaokuwapo baadaye."

Waongo Makadiyani. Quran nzima inasema Waislamu waukubali Utume wa haki wa Nabii Muhammad na wa waliopewa Utume KABLA yake; haijasema Quran kattu "waliopewa Utume BAADA yake."

5. Hao wako juu ya uwongozi utokao kwa Mola wao, na hao ndio wenye kuongoka.

اولئك على هدى من ربهم واولئك هم المفلحون ٥

6. Hakika wale waliokufuru (kwa ukaidi tu na inadi) ni sawa kwao ukiwaonya au usiwaonye; hawataamini.

ان الذين كفروا سواء عليهم ءانذرتهم ام لم
تنذرهم لا يؤمنون ٦

7. (Kama kwamba) Mwenyezi Mungu amepiga muhuri juu ya nyoyo zao na juu ya masikio yao; na juu ya macho yao pana kifuniko; basi watakuwa na adhabu kubwa.

ختم الله على قلوبهم وعلى سمعهم وعلى ابصارهم
غشاوة ولهم عذاب عظيم ٧

8. Na katika watu, wako (wanafiki) wasemao: "Tumemwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho"; na hali ya kuwa wao si wenye kuamini.

ومن الناس من يقول امنا بالله وباليوم
الاخر وما هم بمؤمنين ٨

9. Wanatafuta kumdanganya Mwenyezi Mungu na wale walioamini, lakini hawadanganyi ila nafsi zao; nao hawatambui.

يخادعون الله والذين امنوا وما يخدعون الا انفسهم
وما يشعرون ٩

10. Nyoyoni mwao mna maradhi, na Mwenyezi Mungu amewazidishia maradhi (kwa kuwa kila siku yalikuwa yanaongezeka mambo mengine mengine ya Kiislamu ya kuamini na ya kufanya; na ya kuwaudhi kweli kweli). Basi watakuwa na adhabu iumizayo kwa sababu ya kule kusema kwao uwongo.

في قلوبهم مرض فزادهم الله مرضا ولهم عذاب
اليم بما كانوا يكذبون ١٠

11. Na wanapoambiwa: "Msifanye uharibifu ulimwenguni." Husema: "Sisi ni watengezaji."

واذا قيل لهم لا تفسدوا في الارض
قالوا انما نحن مصلحون ١١

12. Hakika wao ndio waharibuji, lakini hawatambui.

الا انهم هم المفسدون ولكن لا يشعرون ١٢

13. Na wanapoambiwa: "Aminini kama walivyoamini watu;" husema: "Oh! Tuamini kama walivoamini wale wapumbavu?" Hakika wao ndio wapumbavu lakini hawajui.

واذا قيل لهم امنوا كما امن الناس قالوا
انؤمن كما امن السفهاء الا انهم هم السفهاء
ولكن لا يعلمون ١٣

---

Zimetajwa Aya namna hizi za kusema 'waliopewa Utume kabla yake' zaidi kuliko mara 20. Hapa tunataja Robo ya mara hizo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | *Al Baqarah* | Aya ya 3 |
| 2. | *An Nisaa* | Aya ya 61, Aya ya 135 na Aya ya 161 |
| 3. | *Ash Shuura* | Aya ya 3 |

Nawatuonyeshe Makadiyani Aya moja tu inayosema: "Waamini — au wanaamini — yaliyoteremshwa BAADA yake (Nabii Muhammad)". Hawataigunduwa kwani haipo Aya hiyo katika Quran. Basi kuamini hivi walivyozua wao — wakazua utume wa Mirza Ghulam — ni ukafiri. Itikadi inayopinga itikadi tuliyoamrishiwa katika Quran ni ukafiri safi kabisa.

8. Katika Aya 3-5 Mwenyezi Mungu Amewataja wenye kuanini kweli, na katika Aya 6-7 Amewataja makafiri kweli kweli. Sasa Anawataja "wanafiki" ambao wakiwa pamoja na Waislamu hujidai kuwa wao ni Waislamu, na wakiwa pamoja na makafiri hukufuru pamoja nao.

13. Mayahudi walikuwa wakiwafanya wale Waislamu waliotoka Makka wakatupa watu wao na mali yao, wakahamia Madina kumfuata Mtume na kuhifadhi dini yao; na wale Waislamu wa Madina ambao waliwapokea Waislamu wa Makka na kuwagawia mali yao, wakiwafanya wote ni wapumbavu.

14. Na wanapokutana na walioamini husema: "Tumeamini"; na wanapokuwa peke yao kwa mashetani wao husema: "Hakika sisi tu pamoja nanyi, tunawacheza shere tu."

وَإِذَا لَقُوا الَّذِينَ آمَنُوا قَالُوا آمَنَّا وَإِذَا خَلَوْا إِلَىٰ
شَيَاطِينِهِمْ قَالُوا إِنَّا مَعَكُمْ إِنَّمَا نَحْنُ مُسْتَهْزِئُونَ ﴿١٤﴾

15. Mwenyezi Mungu atawalipa shere yao na kuwawacha katika upotofu wao wakitangatanga ovyo.

اللَّهُ يَسْتَهْزِئُ بِهِمْ وَيَمُدُّهُمْ فِي طُغْيَانِهِمْ يَعْمَهُونَ ﴿١٥﴾

16. Hao ndio waliokhiari upotofu kuliko uongofu; lakini biashara yao haikupata faida wala hawakuwa wenye kuongoka.

أُولَٰئِكَ الَّذِينَ اشْتَرَوُا الضَّلَالَةَ بِالْهُدَىٰ فَمَا رَبِحَتْ
تِجَارَتُهُمْ وَمَا كَانُوا مُهْتَدِينَ ﴿١٦﴾

17. Mfano wao (hawa wanafiki) ni kama mfano wa wale (wasafiri waliokumbwa na kiza) wakakoka moto, (na) ulipowaonyesha yaliyo pembezoni mwao, Mwenyezi Mungu aliiondoa nuru yao hiyo na kuwawacha katika viza; hawaoni.

مَثَلُهُمْ كَمَثَلِ الَّذِي اسْتَوْقَدَ نَارًا فَلَمَّا أَضَاءَتْ
مَا حَوْلَهُ ذَهَبَ اللَّهُ بِنُورِهِمْ وَتَرَكَهُمْ فِي ظُلُمَاتٍ
لَا يُبْصِرُونَ ﴿١٧﴾

18. Viziwi, mabubu, vipofu; kwa hivyo hawatarejea.

صُمٌّ بُكْمٌ عُمْيٌ فَهُمْ لَا يَرْجِعُونَ ﴿١٨﴾

19. Au (mfano wao pia) ni kama mvua kubwa itokayo mawinguni; ndani yake mkawa mna viza na radi na umeme; wakawa wakitia vidole vyao masikioni mwao kwa ajili ya mingurumo, kwa kuogopa kufa; (na kufanya hivyo hakuwasaidii kitu). Na Mwenyezi Mungu anawajua vyema hao makafiri.

أَوْ كَصَيِّبٍ مِنَ السَّمَاءِ فِيهِ ظُلُمَاتٌ وَرَعْدٌ وَبَرْقٌ
يَجْعَلُونَ أَصَابِعَهُمْ فِي آذَانِهِمْ مِنَ الصَّوَاعِقِ حَذَرَ
الْمَوْتِ وَاللَّهُ مُحِيطٌ بِالْكَافِرِينَ ﴿١٩﴾

20. Unakaribia umeme huo kunyakua macho yao; kila unapowaangazia huenda ndani yake na unapowafanyia giza husimama. Na Mwenyezi Mungu angependa angaliondoa kusikia kwao na kuona kwao. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye uweza juu ya kila kitu.

يَكَادُ الْبَرْقُ يَخْطَفُ أَبْصَارَهُمْ كُلَّمَا أَضَاءَ لَهُمْ مَشَوْا
فِيهِ وَإِذَا أَظْلَمَ عَلَيْهِمْ قَامُوا وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ
لَذَهَبَ بِسَمْعِهِمْ وَأَبْصَارِهِمْ إِنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ
شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٢٠﴾

21. Enyi watu! Mwabuduni Mola wenu ambaye amekuumbeni nyinyi na wale wa kabla yenu; ili mpate kuokoka

يَا أَيُّهَا النَّاسُ اعْبُدُوا رَبَّكُمُ الَّذِي خَلَقَكُمْ وَالَّذِينَ
مِنْ قَبْلِكُمْ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ ﴿٢١﴾

22. (Mwenyezi Mungu) Ambaye amekufanyieni hii ardhi kuwa kama busati (mliotandikiwa mstarehe), na mbingu kuwa kama paa, na akateremsha maji kutoka mawinguni; na kwa hayo akatoa matunda yawe riziki zenu. Basi msimfanyizie Mwenyezi Mungu washirika, na hali nyinyi mnajua (kuwa hana mshirika).

الَّذِي جَعَلَ لَكُمُ الْأَرْضَ فِرَاشًا وَالسَّمَاءَ بِنَاءً
وَأَنْزَلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَأَخْرَجَ بِهِ مِنَ الثَّمَرَاتِ
رِزْقًا لَكُمْ فَلَا تَجْعَلُوا لِلَّهِ أَنْدَادًا وَأَنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٢٢﴾

---

14. Mashetani wao ni wale wakubwa wao waliokuwa wakiwapoteza. Na wameitwa mashetani kwa sababu mashetani ndio wanaopoteza watu.

17. Aya hizi zinaonyesha nafuu wanayoipata wanafiki hapa ulimwenguni kwa unafiki wao. Na zinaonyesha hali watakayokuwa watakapokufa. Na pia ni mfano wao kwa kuacha kufuata nuru ya Uislamu wakaingia katika viza vya ukafiri.

19, 20. Aya hizi zinaonyesha mfano wa wanafiki namna wanavyokuwa wanaposikia mawaidha na makamio ya Quran. Zile hoja kali kali na utisho wa malipo mabaya watakayolipwa, walikuwa wakiona kama kiza na radi na umeme.

22. Quran haisemi kuwa ulimwengu umeumbwa namna ya busati au tandiko kama wanavyodhania watu

23. Na ikiwa mna shaka kwa hayo tuliyomteremshia Mtumwa Wetu (kuwa hakuteremshiwa na Mwenyezi Mungu), basi leteni sura moja iliyofanywa na (mtu) aliye mfano wake, na muwaite waungu wenu bighairi ya Mwenyezi Mungu (wakusaidieni); ikiwa mnasema kweli.

وَإِن كُنتُمْ فِي رَيْبٍ مِّمَّا نَزَّلْنَا عَلَىٰ عَبْدِنَا فَأْتُوا بِسُورَةٍ مِّن مِّثْلِهِ وَادْعُوا شُهَدَاءَكُم مِّن دُونِ اللَّهِ إِن كُنتُمْ صَادِقِينَ ﴿٢٣﴾

24. Na msipofanya — na hakika hamtafanya kamwe — basi uogopeni moto ambao kuni zake ni watu na mawe, uliowekewa makafiri.

فَإِن لَّمْ تَفْعَلُوا وَلَن تَفْعَلُوا فَاتَّقُوا النَّارَ الَّتِي وَقُودُهَا النَّاسُ وَالْحِجَارَةُ ۖ أُعِدَّتْ لِلْكَافِرِينَ ﴿٢٤﴾

25. Na wabashirie walioamini na kufanya vitendo vizuri, kwamba watapata mabustani yapitayo mito mbele yake; kila mara watakapopewa matunda humo kuwa ni chakula watasema: "Haya ndiyo yale tuliyopewa zamani (ulimwenguni)." Kwani wataletewa (matunda hayo) hali ya kuwa yamefanana (na yale waliyokuwa wakiyajuwa ulimwenguni. Wataletewa kwa sura hiyo; lakini utamu mwingine kabisa): na humo watapata wake waliotakasika (na kila mabaya na machafu); na watakaa milele humo.

وَبَشِّرِ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ أَنَّ لَهُمْ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِن تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ ۖ كُلَّمَا رُزِقُوا مِنْهَا مِن ثَمَرَةٍ رِّزْقًا ۙ قَالُوا هَٰذَا الَّذِي رُزِقْنَا مِن قَبْلُ ۖ وَأُتُوا بِهِ مُتَشَابِهًا ۖ وَلَهُمْ فِيهَا أَزْوَاجٌ مُّطَهَّرَةٌ ۖ وَهُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿٢٥﴾

26. Hakika Mwenyezi Mungu haoni haya kutoa mfano wowote wa mbu na ulio wa zaidi yake. Ama wale wanaoamini, wao hujua ya kwamba hiyo ni haki iliyotoka kwa Mola wao; lakini wale waliokufuru husema: "Ni nini analotaka Mwenyezi Mungu kwa mfano huu?" (Mwenyezi Mungu) huwawachia wengi kupotea kwa mfano huo na huwaongoza wengi kwa mfano huo pia; lakini hamwachii yo yote kupotea kwa mfano huo (na mwingineo) isipokuwa wale wavunjao amri (Zake)

إِنَّ اللَّهَ لَا يَسْتَحْيِي أَن يَضْرِبَ مَثَلًا مَّا بَعُوضَةً فَمَا فَوْقَهَا ۚ فَأَمَّا الَّذِينَ آمَنُوا فَيَعْلَمُونَ أَنَّهُ الْحَقُّ مِن رَّبِّهِمْ ۖ وَأَمَّا الَّذِينَ كَفَرُوا فَيَقُولُونَ مَاذَا أَرَادَ اللَّهُ بِهَٰذَا مَثَلًا ۘ يُضِلُّ بِهِ كَثِيرًا وَيَهْدِي بِهِ كَثِيرًا ۚ وَمَا يُضِلُّ بِهِ إِلَّا الْفَاسِقِينَ ﴿٢٦﴾

---

wengine. Muradi wa maneno haya, katika Aya hii na nyinginezo, ni kuwa Mwenyezi Mungu Ameikunjua Ardhi hata viumbe wakaweza kuishi kwa raha na kufanya haja zao bila ya taklifu juu yake. Na samaa hapa ni mawingu kama yalivyotajwa katika sura nyengine kwa jina la sahab (mawingu). Sahab ndiyo mawingu na samaa ni kila kilicho juu yako. Basi tamko la samaa inapotajwa mvua lina maana ya lile tamko la sahab. Siyo mvua inatoka mbinguni. Wenyewe kwa macho yetu tukipanda ndege (aeroplane) tunaiona haitoki mbinguni.

23. Makafiri walikuwa wakikanusha Quran na kudai kuwa ni maneno yake yeye Muhammad, si maneno ya Mungu. Basi hapa Mwenyezi Mungu Anawatahayarisha na kuwaambia kwamba Muhammad ni mwanadamu kama nyinyi. Basi kama yeye ameweza kutunga maneno kama haya kwa nini nyinyi hamwezi? Jaribuni na muwaite hao waungu wenu wakupeni msaada.

24. Hapa Mwenyezi Mungu Anawakatia kuwa hawataweza kufanya hilo, na Anawatahadharisha na Adhabu yake.

Wamesema katika maelezo ya tafsiri ya Aya mbili hizi — walizozifanya kuwa ni 25 na 26 — kuwa maisha ya Akhera ni ya Kiroho tu si ya Kiwiliwili.

Hivi sivyo unavyosema Uislamu. Uislamu unasema kuwa "Maisha ya Akhera ni ya Roho na Kiwiwili, si ya Roho tu". Tamko gani liliowafahamisha — katika Aya mbili hizi au nyinginezo — kuwa hayo ni maisha ya kiroho tu? Yo yote anayeyasoma maneno ya Quran na ya Hadithi za Mtume anaona waziwazi kuwa yamekhusu roho na kiwiliwili. Nawatuonyeshe NENO la Mwenyezi Mungu au Mtume linalosema kuwa maisha ya huko ni ya Kiroho tu.

Basi kuamini kwao hivyo ni kinyume cha ilivyosema Quran na Hadithi za Mtume.

25. Kubashiria ni kuwapa khabari ya furaha.

26. Mwenyezi Mungu alipowapigia mfano waungu wao batili kuwa (a) Hawawezi kuumba hata nzi bali hata

27. Wanaovunja ahadi ya Mwenyezi Mungu baada ya kuifunga na kuyakata aliyoamrisha Mwenyezi Mungu kuungwa, na kufanya ufisadi katika ardhi. Hao ndio wenye khasara.

الَّذِينَ يَنقُضُونَ عَهْدَ اللَّهِ مِن بَعْدِ مِيثَاقِهِ
وَيَقْطَعُونَ مَا أَمَرَ اللَّهُ بِهِ أَن يُوصَلَ وَيُفْسِدُونَ
فِي الْأَرْضِ أُولَٰئِكَ هُمُ الْخَاسِرُونَ ﴿٢٧﴾

28. Vipi mnamkanusha Mwenyezi Mungu, na hali mlikuwa wafu, akakuhuisheni; kisha atakufisheni; kisha atakuhuisheni; kisha kwake mtarejeshwa (atakapokufufueni).

كَيْفَ تَكْفُرُونَ بِاللَّهِ وَكُنتُمْ أَمْوَاتًا فَأَحْيَاكُمْ
ثُمَّ يُمِيتُكُمْ ثُمَّ يُحْيِيكُمْ ثُمَّ إِلَيْهِ تُرْجَعُونَ ﴿٢٨﴾

29. Yeye ndiye aliyekuumbieni vyote vilivyomo katika ardhi (kabla hajakuumbeni ili mkute kila kitu tayari), tena akakusudia kuumba mbingu; na akazifanya mbingu saba. Naye ndiye ajuaye kila kitu.

هُوَ الَّذِي خَلَقَ لَكُم مَّا فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا ثُمَّ اسْتَوَىٰ
إِلَى السَّمَاءِ فَسَوَّاهُنَّ سَبْعَ سَمَاوَاتٍ
وَهُوَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿٢٩﴾

30. (Wakumbushe watu khabari hii;) Wakati Mola wako alipowaambia Malaika: "Mimi nitaleta viumbe vyengine kukaa katika ardhi." (Nao ndio wanaadamu). Wakasema (Malaika): "Utaweka humo watakaofanya uharibifu humo na kumwaga damu, hali sisi tunakutukuza kwa sifa zako na kukutaja kwa utakatifu wako?" Akasema (Mwenyezi Mungu): "Hakika Mimi nayajua msiyoyajua."

وَإِذْ قَالَ رَبُّكَ لِلْمَلَائِكَةِ إِنِّي جَاعِلٌ فِي الْأَرْضِ
خَلِيفَةً قَالُوا أَتَجْعَلُ فِيهَا مَن يُفْسِدُ فِيهَا وَيَسْفِكُ
الدِّمَاءَ وَنَحْنُ نُسَبِّحُ بِحَمْدِكَ وَنُقَدِّسُ لَكَ
قَالَ إِنِّي أَعْلَمُ مَا لَا تَعْلَمُونَ ﴿٣٠﴾

31. Na (Mwenyezi Mungu) akamfundisha (Nabii) Adam majina ya vitu vyote, kisha akaviweka mbele ya Malaika, na akasema (kuwaambia Malaika): "Niambieni majina ya vitu hivi ikiwa mnasema kweli (kuwa nyinyi ndio wajuzi wa mambo)."

وَعَلَّمَ آدَمَ الْأَسْمَاءَ كُلَّهَا ثُمَّ عَرَضَهُمْ عَلَى الْمَلَائِكَةِ
فَقَالَ أَنبِئُونِي بِأَسْمَاءِ هَٰؤُلَاءِ إِن كُنتُمْ صَادِقِينَ ﴿٣١﴾

---

hawawezi kumfukuza na kuwa (b) Anayewategemea ni kama buibui anayetegemea nyumba yake ile isiyokuwa na maana, Makafiri walisema "Mwenyezi Mungu na ukubwa wake wote huo atataja mfano wa nzi na buibui?"

27. Muradi wa kuvunja ahadi ya Mwenyezi Mungu hapa ni kule kumkadhibisha Mtume Muhammad baada ya kumjua kuwa ndiye Mtume aliyebashiriwa katika vitabu vyao. Basi hawa ndio anaowaachilia kupotea na walio kama hawa kama ilivyo katika aya 86 ya Al Imran, aya 27 ya Surat Ibrahim, aya 34 na 74 za Suratul Muumin na nyenginezo.

30. Aya hii inafahamisha kuwa kabla ya wanaadamu kulikuwa na viumbe wengine katika ulimwengu lakini Mwenyezi Mungu hakututajia jinsi yao na namna yao.

Amezua (Mkadiyani) katika maelezo ya Aya walioifanya ni Aya 31 kuwa Nabii Adam huyu aliyetajwa katika Quran (a) siye asili ya wanaadamu sisi, na kuwa (b) yeye Adam ni kizazi cha chungu ya Maadamu chungu nzima waliopita.

Na walipoikosa Aya ya kuipotoa katika jambo hili au Hadithi ya kuipotoa, na neno la mwanachuoni wa kutegemewa la kulipotoa katika jambo hili, wametaja neno la Muhyiddin ibn Araby; na hali ya kuwa wanajua kuwa hapana ruhusa kufuata maneno yaliyomo katika vitabu vya huyu Muhyiddin ibn Araby. Maneno ya kufuatwa ni ya Sheikh Abubakr ibn Araby. Maneno ya Muhyiddin yanaitakidiwa kuwa yameingia ndani yake maneno yasiyokuwa ya haki; kwa hivyo hapana hata ruhusa ya kusoma cho chote kile katika vitabu vyake. Wanavyuoni wetu wote wa kutegemewa wamesema haya — na yeye mfasiri wa Makadiyani anajua, lakini anataka tu kupoteza Waislamu.

Katika walioharimisha kusoma vitabu vya huyu Muhyiddin Araby ni bwana mkubwa kabisa na mtungaji mashuhuri mtegemewa — Sayyid Abdalla al Haddad. Aliyeyataja haya katika sahifa 11 ya kitabu chake mashuhuri kinachokubaliwa ulimwengu mzima na kinachosomwa sana hapa pia, kinachoitwa *Risalatul Muawana*.

31. Wamesema — kwenye Aya waliofanya ya 32 — kuwa *Al Asmaa*, ni majina ya Mungu kama ilivyo katika

32. Wakasema (Malaika): "Utakatifu ni wako! Hatuna ilimu isipokuwa ile uliyotufundisha; bila shaka wewe ndiye Mjuzi na ndiye Mwenye hikima." (Mwenye kuweka kila kitu mahala pake).

قَالُوا سُبْحَانَكَ لَا عِلْمَ لَنَا إِلَّا مَا عَلَّمْتَنَا ۖ إِنَّكَ أَنْتَ الْعَلِيمُ
الْحَكِيمُ ﴿٣٢﴾

33. Akasema (Mwenyezi Mungu): "Ewe Adam! Wambie majina yake." Alipowaambia majina yake alisema (Mwenyezi Mungu): "Sikukwambieni kwamba mimi ninajua siri za mbinguni na za ardhi; tena najua mnayoyadhihirisha na mliyokuwa mnayaficha?"

قَالَ يَا آدَمُ أَنْبِئْهُمْ بِأَسْمَائِهِمْ ۖ فَلَمَّا أَنْبَأَهُمْ بِأَسْمَائِهِمْ
قَالَ أَلَمْ أَقُلْ لَكُمْ إِنِّي أَعْلَمُ غَيْبَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ
وَأَعْلَمُ مَا تُبْدُونَ وَمَا كُنْتُمْ تَكْتُمُونَ ﴿٣٣﴾

34. Na (wakumbushe watu khabari hii): Tulipowaambia Malaika: "Msujudieni Adam" (yaani mwadhimisheni kwa ile ilimu yake aliyopewa). Wakamsujudia wote isipokuwa Iblis; akakataa na akajivuna; na (tokea hapo) alikuwa katika makafiri; (ila alichanganyika tu na Malaika).

وَإِذْ قُلْنَا لِلْمَلَائِكَةِ اسْجُدُوا لِآدَمَ فَسَجَدُوا إِلَّا إِبْلِيسَ
أَبَىٰ وَاسْتَكْبَرَ وَكَانَ مِنَ الْكَافِرِينَ ﴿٣٤﴾

35. Na tulisema (baada ya hapo kumwambia Nabii Adam): "Ewe Adam! Kaa wewe na mkeo katika bustani hii (Peponi); na kuleni humo maridhawa po pote mpendapo, lakini msiukaribie mti huu tu; msije kuwa miongoni mwa waliodhulumu (nafsi zao kwa kukhalifu amri za Mwenyezi Mungu)."

وَقُلْنَا يَا آدَمُ اسْكُنْ أَنْتَ وَزَوْجُكَ الْجَنَّةَ وَكُلَا مِنْهَا
رَغَدًا حَيْثُ شِئْتُمَا وَلَا تَقْرَبَا هَٰذِهِ الشَّجَرَةَ فَتَكُونَا
مِنَ الظَّالِمِينَ ﴿٣٥﴾

---

Aya ya 180 ya sura ya Saba (yaani *Suratul Aaraf* Juzuu ya 9) yaani *Walillahil Asmaul Husna*. Tunawaambia Itakuwaje Majina ya Mwenyezi Mungu kutandazwa yakadhihirishwa? Hayo ni majina ya vitu vyenye roho na visivyokuwa na roho, vilivyowekwa mbele ya Nabii Adam akaambiwa avitaje. Na hivyo kutumiwa *'Him'* badala ya *'Ha'* ni kwa sababu vimechanganyika visivyokuwa na akili na vyenye akili. Na hii ndiyo :asturi ya lugha ya Kiarabu. Labda hafahamu lugha barabara; anajua juu juu tu. Na hii ndiyo khatari ya ilimu chache. Ilimu chache udhia: Ilimu chache yadhuru. Na wanaona hapo imeandikwa 'Asmai haaulai' — majina ya hawa. Iko wapi majina ya Mwenyezi Mungu?

35. Mke wa Adam ni Hawwaa. Na Quran haikusema kwa uwazi namna alivyoumbwa. Na huo mti pia hatukuambiwa ni mti gani.

Wamevuruga Makadiyani Aya waliyoifanya ya 36 mahala pawili (1) Wamesema kuwa hakuwako Peponi Nabii Adam hapo alipoumbwa wala mkewe—Bibi Hawwaa. Lakini waliumbwa hapa ulimwenguni Babylon (Iraq au Assyria) Na maneno yao khasa waliyoyatia katika hiyo tafsiri yao ni haya: "Hapa neno hili maana yake si Pepo bali ni bustani ya hapa duniani . . . Uchunguzi wa siku hizi umebainisha ya kuwa mahala alipowekwa Adamu ni katika bustani ya Eden iliyokuwa karibu na Babylon katika nchi ya Iraq au Assyria."

Tazama wanavyoipinga Quran dhahir shahir. Quran inasema katika Aya ya 36 *Suratul Baqarah* (wao wameifanya ya 37) na katika Aya 24 ya *Suratul Aaraf* (ambayo wao wameifanya ya 25) na nyinginezo kuwa: "Shukeni. Na kao lenu litakuwa katika ardhi, na starehe yenu pia." Hapa Mwenyezi Mungu anasema "Watoke kwenye Pepo Wende katika ardhi". Wao Makadiyani wanasema kuwa walikuwa papa hapa katika ardhi na Pepo hii ilikuwa katika ardhi! Natutahadhari na kutolewa maanani na Makadiyani.

(2) Na mahala pa pili walipopaharibu kusudi katika Aya hii ni kusema kuwa lile tamko la *Shajarah* (mti)linalosema *'Walaa Taqrabaa Hadhihish Shajara'* (yaani Msiukurubie mti huu). Wana mambo mabaya.' Hivi ndivyo walivyosema Makadiyani na wakasema kuwa tafsiri hiyo wameitoa katika kamusi la Lane (yaani Arabic English Lexicon by E.W. Lane).

Tazama hamu yao hii ya kutaka kuwapoteza Waislamu na dini yao ya haki. Wanajitahidi kila namna kugeuza tafsiri ya Quran, kama wanavyopoteza tafsiri ya Hadithi za Mtume na maneno ya wanavyuoni wa haki. Mwanzo wa tafsiri yao (viii) wametaja chungu ya majina ya tafsiri za Quran kuonyesha kuwa wametegemea tafsiri hizo

36. (Lakini) Shetani (yule Iblis adui yao) aliwatelezesha wote wawili (wakakhalifu amri ile, wakala katika mti huo waliokatazwa) na akawatoa katika ile (hali) waliyokuwa nayo. Tukawaambia: "Nendeni, hali ya kuwa maadui nyinyi kwa nyinyi, na makazi yenu (sasa) katika ardhi, na (mtapata) starehe humo kwa muda (makhususi)."

فَأَزَلَّهُمَا الشَّيْطَٰنُ عَنْهَا فَأَخْرَجَهُمَا مِمَّا كَانَا فِيهِ
وَقُلْنَا اهْبِطُوا بَعْضُكُمْ لِبَعْضٍ عَدُوٌّ وَلَكُمْ فِي الْأَرْضِ
مُسْتَقَرٌّ وَمَتَٰعٌ إِلَىٰ حِينٍ ﴿٣٦﴾

37. Kisha Adam akapokea maneno (ya maombi) kwa Mola wake, (akaomba), na Mola wake akapokea toba yake; hakika yeye ndiye mwingi wa kupokea toba (kwa wenye kutubia) na Mwingi wa kurehemu (kwa wanaostahiki kurehemewa. Ama Iblis hakutubia kwa hivyo hakustahiki kurehemewa).

فَتَلَقَّىٰ آدَمُ مِن رَّبِّهِ كَلِمَٰتٍ فَتَابَ عَلَيْهِ إِنَّهُ هُوَ
التَّوَّابُ الرَّحِيمُ ﴿٣٧﴾

38. Tukasema: "Shukeni humo nyote; na kama ukikufikieni uwongozi utokao kwangu, basi watakaofuata uwongozi wangu huo haitakuwa khofu juu yao wala hawatahuzunika."

قُلْنَا اهْبِطُوا مِنْهَا جَمِيعًا فَإِمَّا يَأْتِيَنَّكُم
مِّنِّي هُدًى فَمَن تَبِعَ هُدَايَ فَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ
وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿٣٨﴾

39. "Lakini wenye kukufuru na kuyakadhibisha maneno yetu, hao ndio watakaokuwa watu wa Motoni, humo watakaa milele."

وَالَّذِينَ كَفَرُوا وَكَذَّبُوا بِآيَٰتِنَا أُولَٰئِكَ أَصْحَٰبُ
النَّارِ هُمْ فِيهَا خَٰلِدُونَ ﴿٣٩﴾ ع

40. Enyi kizazi cha Israili (Nabii Yaaqub! Yaani Ee Mayahudi!) Zikumbukeni neema zangu nilizokuneemesheni; na tekelezeni ahadi yangu (ya kuwa akija Mtume mtamfuata), nitatekeleza ahadi yenu (ya kukupeni Pepo); na niogopeni mimi tu.

يَٰبَنِي إِسْرَٰٓءِيلَ اذْكُرُوا نِعْمَتِيَ الَّتِي أَنْعَمْتُ عَلَيْكُمْ
وَأَوْفُوا بِعَهْدِي أُوفِ بِعَهْدِكُمْ وَإِيَّٰيَ فَارْهَبُونِ ﴿٤٠﴾

---

katika kufasiri kwao. Basi kwa nini wasimtaje mmoja katika wafasiri hao kuwa yeye ndiye waliyemtegemea katika kufasiri *Shajarah* kwa ugomvi? Wana yakini kuwa hakuna mfasiri mmoja katika hao na wengineo aliyefasiri hivi. Wote hao wamefasiri *Shajarah* kuwa mti. Na vile vile wametaja majina ya baadhi ya Maqamusi ambayo yametungwa makusudi kwa kufasiri maneno yaliyomo katika Quran tu, kama hiyo Mufradat waliyoitaja. Na kama *Kalimatul Quran* na kama *Majazul Quran*. Kwa nini wasikitaje kimoja katika hivi kilichofasiri tamko hili la Shajarah kuwa maana yake ugomvi? Wanajua yakini kuwa hapana mmoja aliyelifasiri tamko hilo kuwa maana yake ugomvi. Kataja kamus la Lane lisilokhusika na maana ya maneno ya Quran, bali limekhusika na maneno ya Kiarabu tu. Na juu ya hivi huyo Lane hakusema tamko la Shajarah kwa Jimu yenye fat-ha kuwa maana yake ugomvi. Makamus husema tamko la shajr (kwa Jimu yenye sukuni) ndiyo ugomvi. na wao wanajua kuwa hivi ndivyo ilivyo katika hilo kamus la Lane kama Makamus mengine, kama vile Al Qamus, Al Munjid na mengineyo. Lakini wanataka tu kuwapoteza Waislamu makusudi. Hata lugha yetu ya Kiswahili inakuwa vivi hivi. Kwa kugeuka IRABU inageuka maana. Kiti, Kito, Kitu ni zenye maana mbali mbali kabisa, na zote zina harufu zile zile na irabu zile zile, ila ile irabu ya mwisho tu. Na vile vile Kati, Kiti na Koti, ile irabu ya mwanzo ndiyo iliyopelekea kuwa maana mbali. Na vile vile Kuti na Kutu na Kuta na hama na hema na homa, na chama na chema na chuma. Wanajua hawa, lakini hamu yao kuwapoteza tu Waislamu na dini yao ya haki.

37. Maneno aliyopokea Adam kwa Mola Wake ni haya "Mola wetu! Tumedhulumu nafsi zetu; kama hutusamehe na kuturehemu bila shaka tutakuwa miongoni mwa wenye khasara." Taz Sura 7 *(Al Aaraf)* Aya 23.

40. Neema walizoneemeshwa Mayahudi ni nyingi, Taz. Aya 47 na 49-50. Na hapa wanasemezwa kwa mujibu wa itikadi zao wenyewe, wanaambiwa: Mnadai kuwa nyinyi ndio mlioneemeshwa na Mwenyezi Mungu: basi jee, mbona mmezisahau neema zangu? Mnadai kuwa mmefanyiana ahadi na mimi: basi Mimi nimekwisha kutimizieni ahadi yangu kwa kukutoweni katika nchi ya tabu na mashaka, na kukupeni Kanaan, nchi yenye "kuchuruzika maziwa na asali." Je nyinyi mmetimiza vipi ahadi yenu?

41. Na aminini niliyoyateremsha ambayo yanasadikisha yaliyo pamoja nanyi, wala msiwe wa kwanza kuyakataa. Wala msiyauze maneno yangu kwa ajili ya thamani ndogo tu (ya kilimwenguni); na niogopeni Mimi tu.

وَآمِنُوا بِمَا أَنزَلْتُ مُصَدِّقًا لِّمَا مَعَكُمْ وَلَا تَكُونُوا أَوَّلَ كَافِرٍ بِهِ ۖ وَلَا تَشْتَرُوا بِآيَاتِي ثَمَنًا قَلِيلًا وَإِيَّايَ فَاتَّقُونِ ﴿٤١﴾

42. Wala msichanganye haki na batili, na mkaficha haki, na hali mnajua.

وَلَا تَلْبِسُوا الْحَقَّ بِالْبَاطِلِ وَتَكْتُمُوا الْحَقَّ وَأَنتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٤٢﴾

43. Na simamisheni Sala (Enyi Mayahudi) na toeni Zaka na inameni pamoja na wanaoinama (yaani kuweni Waislamu).

وَأَقِيمُوا الصَّلَوٰةَ وَآتُوا الزَّكَوٰةَ وَارْكَعُوا مَعَ الرَّاكِعِينَ ﴿٤٣﴾

44. Je! Mnawaamrisha watu kutenda mema na mnajisahau nafsi zenu, hali mnasoma Kitabu (cha Mwenyezi Mungu kuwa kufanya hivyo ni vibaya)? Basi je, hamfahamu?

أَتَأْمُرُونَ النَّاسَ بِالْبِرِّ وَتَنسَوْنَ أَنفُسَكُمْ وَأَنتُمْ تَتْلُونَ الْكِتَابَ ۚ أَفَلَا تَعْقِلُونَ ﴿٤٤﴾

45. Na jisaidieni (katika mambo yenu) kwa kusubiri na kwa kusali; na kwa hakika jambo hilo ni gumu isipokuwa kwa wanyenyekevu

وَاسْتَعِينُوا بِالصَّبْرِ وَالصَّلَوٰةِ ۚ وَإِنَّهَا لَكَبِيرَةٌ إِلَّا عَلَى الْخَاشِعِينَ ﴿٤٥﴾

46. Ambao wana yakini ya kwamba watakutana na Mola wao na ya kwamba watarejea Kwake.

الَّذِينَ يَظُنُّونَ أَنَّهُم مُّلَاقُو رَبِّهِمْ وَأَنَّهُمْ إِلَيْهِ رَاجِعُونَ ﴿٤٦﴾

47. Enyi kizazi cha Israili (Mayahudi)! Kumbukeni neema zangu nilizokuneemesheni, na nikakutukuzeni kuliko viumbe wengine (wa wakati huo).

يَا بَنِي إِسْرَائِيلَ اذْكُرُوا نِعْمَتِيَ الَّتِي أَنْعَمْتُ عَلَيْكُمْ وَأَنِّي فَضَّلْتُكُمْ عَلَى الْعَالَمِينَ ﴿٤٧﴾

48. Na iogopeni Siku ambayo nafsi haitaifaa nafsi nyingine cho chote, wala hayatakubaliwa kwake (nafsi hiyo) maombezi (kama ataombewa), wala hakitapokewa kikomboleo kwake; wala hawatanusuriwa.

وَاتَّقُوا يَوْمًا لَّا تَجْزِي نَفْسٌ عَن نَّفْسٍ شَيْئًا وَلَا يُقْبَلُ مِنْهَا شَفَاعَةٌ وَلَا يُؤْخَذُ مِنْهَا عَدْلٌ وَلَا هُمْ يُنصَرُونَ ﴿٤٨﴾

49. Na (kumbukeni) Tulipokuokoeni kwa watu wa Firauni waliokupeni adhabu mbaya; wakiwachinja watoto wenu wanaume na kuwawacha hai wanawake; na katika hayo (kuokolewa huko) ilipatikana neema kubwa iliyotoka kwa Mola wenu.

وَإِذْ نَجَّيْنَاكُم مِّنْ آلِ فِرْعَوْنَ يَسُومُونَكُمْ سُوءَ الْعَذَابِ يُذَبِّحُونَ أَبْنَاءَكُمْ وَيَسْتَحْيُونَ نِسَاءَكُمْ ۚ وَفِي ذَٰلِكُم بَلَاءٌ مِّن رَّبِّكُمْ عَظِيمٌ ﴿٤٩﴾

---

41. Ahadi waliyopewa Mayahudi katika *Taurati* ni kuwa Mwenyezi Mungu Atawaletea Nabii Amtie Maneno Yake katika kinywa chake, na awaambie kila alilomwusia; na Mwenyezi Mungu Akamleta Mtume Muhammad akawaambia kwa ulimi wake alilotumwa na Mwenyezi Mungu. Hili linathibitisha yale yaliyosemwa katika *Taurati*, kwa sababu hakuja Nabii mwengine aliyekuwa na sifa hizo zilizomo katika *Taurati*. Kama Nabii Muhammad angekuwa muongo angeuliwa kama ilivyosemwa katika Marejezo 18: 18-22. Kwa kutaka utukufu wa Ulimwenguni Mayahudi walizikataa dalili hizo wakazibadilisha kwa thamani ndogo, wakaficha haki.

44. Baadhi ya wanavyuoni wa Kiyahudi wakisilimu jamaa zao wakapata habari, huwaendea kwa siri wakawaambia 'Dini hii mliyoifuata aliyokuja nayo Nabii Muhammad ni ya haki, shikamaneni nayo; lakini sisi hatuwezi kukosa ukubwa wetu.' Ndiyo Mwenyezi Mungu anawasimanga kwa Aya hii.

45. Ingawa maneno haya wanaambiwa Mayahaudi lakini yanawahusu watu wote kama ilivyo ada ya Quran. Subira imesifiwa mara nyingi katika Quran. Mtu akisubiri katika kuendelea na mema aliyoamrishwa na katika kuacha mabaya anayoyapenda, na akasubiri juu ya mashaka na tabu za ulimwenguni, bila shaka atafaulu duniani na Akhera.

وإذ فرقنا بكم البحر فأنجيناكم وأغرقنا
آل فرعون وأنتم تنظرون ﴿٥٠﴾

50. Na (kumbukeni) tulipoitenga bahari kwa ajili yenu na tukakuokoeni, na tukawazamisha watu wa Firauni, na hali mkitazama.

وإذ واعدنا موسى أربعين ليلة ثم اتخذتم
العجل من بعده وأنتم ظالمون ﴿٥١﴾

51. Na (kumbukeni) tulipomwahidi Musa siku arubaini, (afanye ibada mfululizo, kisha tumpe Taurati). Mkamfanya ndama (kuwa mungu) baada yake, na mkawa madhalimu (wa nafsi zenu).

ثم عفونا عنكم من بعد ذلك لعلكم تشكرون ﴿٥٢﴾

52. Kisha tukakusameheni baada ya hayo, ili mpate kushukuru.

وإذ آتينا موسى الكتاب والفرقان لعلكم
تهتدون ﴿٥٣﴾

53. Na (kumbukeni) Tulipompa Musa Kitabu (kilichokusanya kila wanayoyahitajia) na cha kupambanua baina ya yaliyo ya haki na yasiyokuwa ya haki ili mpate kuongoka.

وإذ قال موسى لقومه يا قوم إنكم ظلمتم
أنفسكم باتخاذكم العجل فتوبوا إلى بارئكم فاقتلوا
أنفسكم ذلكم خير لكم عند بارئكم فتاب
عليكم إنه هو التواب الرحيم ﴿٥٤﴾

54. Na (kumbukeni habari hii:) Musa alipowaambia watu wake: "Enyi watu wangu! Hakika nyinyi mmezidhulumu nafsi zenu kwa kumfanya kwenu ndama (kuwa mungu). Basi tubuni kwa Mwumba Wenu (Mola wenu) na ziueni nafsi zenu; haya ni bora kwenu mbele ya Mwumba wenu." Basi akapokea toba yenu. Hakika Yeye ndiye apokeaye toba na ndiye Mwenye kurehemu.

وإذ قلتم يا موسى لن نؤمن لك حتى نرى الله
جهرة فأخذتكم الصاعقة وأنتم تنظرون ﴿٥٥﴾

55. Na (kumbukeni habari hii pia:) Mliposema: "Ewe Musa! Hatutakuamini mpaka tumwone Mwenyezi Mungu waziwazi." Yakakunyakueni mauti ya ghafla (ya kukuueni moto wa radi), na hali mnaona.

ثم بعثناكم من بعد موتكم لعلكم تشكرون ﴿٥٦﴾

56. Kisha tukakufufueni baada ya kufa kwenu, ili mpate kushukuru.

---

50. Aya hii ni ya Kuwakumbusha Mayahudi wakati wazee wao walipokuwa wanatoka Misri kumkimbia Firauni, Mwenyezi Mungu akawapasulia bahari wakapita kwa salama.

51. Aya hii ni ya kuwakumbusha ubaya wa wazee wao: Nabii Musa aliwaaga kuwa ataondoka muda wa siku 40, atakaporejea atawaletea Kitabu cha Sharia yao kinachotoka kwa Mwenyezi Mungu.

Basi baada ya siku chache tu tangu kuondoka Nabii Musa waliacha kumwabudu Mwenyezi Mungu, wakatengeneza ndama wa dhahabu wakawa wanamuabudu. Soma hadithi yao katika Sura *Taa Haa* 20: 87-97.

53. "Cha kupambanua", muradi wake ni ile miujiza aliyopewa Nabii Musa iliyopambanua baina ya haki na batili.

54. Kwa makosa makubwa waliyofanya Mayahudi ya kuabudu ndama Mwenyezi Mungu Aliwapa adabu hii ya kuuana wenyewe kwa wenyewe.

55. Kisa cha Mayahudi kutaka kumwona Mwenyezi Mungu waziwazi kinatajwa pia katika Talmud.

56. Wameivuruga Aya waliyoihisabu kuwa ni ya 57 Wakasema kuwa Hawakufa watu hao kisha wakafufuliwa kwani wanaokufa hawafufuki mpaka siku ya Kiyama. Nao wanajua kwa yakini — na Waislamu wote wanajua kwa yakini—kuwa katika Miujiza ya Nabii Isa ni kuwa alifufua baadhi ya waliokuwa wamekufa, kisha wakafa tena papo hapo baada ya kuthibitika Muujiza huo mbele ya wote waliokuwa hapo. Mwenyezi Mungu ameitaja katika Aya nyingi za Quran habari hii na kama hii; kama Aya ya 49 ya *Surat Aali Imran* (wao wameihisabu ya 50); na wameifasiri hivi:- "Na kuwahuisha wafu" . . . na kama Aya ya 110 ya *Suratul Maida* (wao wameihisabu ya 111), na wameifasiri hivi:- "Na ulipowatoa wafu."

57. Na tukakutilieni kivuli kwa mawingu (mlipokuwa mnakata jangwa kutoka Misri kwenda Sham) na tukakuteremshieni Manna na Salwa: (tukakwambieni) "Kuleni katika vitu vizuri hivi tulivyokuruzukuni." Nao hawakutudhulumu Sisi (walipokhalifu amri Yetu) lakini walikuwa wamejidhulumu nafsi zao (kwa huko kuacha kututii).

وَظَلَّلْنَا عَلَيْكُمُ الْغَمَامَ وَأَنْزَلْنَا عَلَيْكُمُ الْمَنَّ
وَالسَّلْوَىٰ كُلُوا مِنْ طَيِّبَاتِ مَا رَزَقْنَاكُمْ وَمَا ظَلَمُونَا
وَلَٰكِنْ كَانُوا أَنْفُسَهُمْ يَظْلِمُونَ ﴿٥٧﴾

58. Na (kumbukeni khabari hii vile vile:) Tuliposema: "Ingieni mji huu, na humo kuleni kwa maridhawa po pote mpendapo, na ingieni katika mlango wake kwa kunyenyekea, na semeni. "Tusamehe dhambi zetu". Tutakusameheni makosa yenu, na tutawazidishia wema wale wafanyao wema.

وَإِذْ قُلْنَا ادْخُلُوا هَٰذِهِ الْقَرْيَةَ فَكُلُوا مِنْهَا حَيْثُ
شِئْتُمْ رَغَدًا وَادْخُلُوا الْبَابَ سُجَّدًا وَقُولُوا حِطَّةٌ
نَغْفِرْ لَكُمْ خَطَايَاكُمْ وَسَنَزِيدُ الْمُحْسِنِينَ ﴿٥٨﴾

59. (Lakini wale) waliodhulumu (nafsi zao) walibadili kauli isiyokuwa waliyoambiwa. (Badala ya kuomba wasamehewe makosa yao na hawatafanya tena, ndipo walipozidi ubaya). (Kwa hivyo) tukaiteremsha juu ya wale waliodhulumu adhabu kubwa kutoka mbinguni kwa sababu ya kuasi kwao.

فَبَدَّلَ الَّذِينَ ظَلَمُوا قَوْلًا غَيْرَ الَّذِي قِيلَ لَهُمْ
فَأَنْزَلْنَا عَلَى الَّذِينَ ظَلَمُوا رِجْزًا مِنَ السَّمَاءِ
بِمَا كَانُوا يَفْسُقُونَ ﴿٥٩﴾ ع

---

Na ziko Aya nyingine pia za kuonyesha miujiza ya kufufuliwa waliokufa. Wao Makadiyani wanasema kuwa Quran imesema waliokufa hawafufuki mpaka Siku ya Kiyama. Lakini na Quran ndiyo iliyosema haya pia. Siyo tuyafuate mengine katika Quran, na mengine tuyatupe! Quran imesema kufufuliwa kwa viumbe wote ni Akhera; na imesema vile vile kuwa wachache kabisa — kwa ajili ya kuonyesha Miujiza — walifufuliwa hapa duniani kwa muda mchache, kisha wakafa vile vile baada ya kuthibiti huo muujiza. Basi lazima tuamini yote yanayosemwa na Quran.

Halafu hapo wakatoa stishhadi za uwongo za kuonyesha kuwa tamko la mauti lina maana nyingine siyo kufa. Wakasema ati tamko la Mait lililomo katika Sura ya 50 (yaani *Surat Qaf*) halionyeshi kufa. Bali linaonyesha (1) kukoma uweza wa kukua. Na hali ya kuwa wao wenyewe katika tafsiri yao katika Aya ya 12 ya Sura hii — kwa mpango wao — wamefasiri: "Tukafufua mji uliokufa." Wakasema na tamko la Mittu lililomo katika Sura ya 19 *(Surat Maryam)* maana yake kutokuwa na fahamu. Na hali ya kuwa wao wenyewe wamelifasiri katika Aya waliyosema kuwa ni ya 12. Walifasiri hivi: "Laiti ningekufa kabla ya haya". Wakasema tena pia kuwa tamko la maiti lililoko katika Sura ya 6 (yaani *Suratul An-Am)* kwenye Aya waliyosema ni ya 123 maana yake (a) kukosa akili. Na wao wenyewe nafsi yao wameifasiri hapa kwa: "Je, aliyekuwa maiti kisha tukamhuisha"? Khalafu wakasema kuwa tamko la mauti lililomo katika Sura ya 14 (yaani *Surat Ibrahim)* katika Aya waliyosema ya 18 maana yake (4) Kulemewa na huzuni, sikitiko au hofu. Na wao wenyewe wameifasiri hivi: "Na mauti yatamfikia . . ." Tena wakasema kuwa tamko la Amwat lililomo katika Sura ya 3 (yaani *Aali Imran)* katika Aya waliyoita ya 170 maana yake kutokuwa na ucha Mungu au kufa kiroho, na wenyewe wameifasiri: "ni wafu". Tena wakatoa tafsiri nyingine za uwongo wasizozitajia Aya za Quran. Lakini inawatosha hizaya kwa hizi walizozitajia Aya za Quran. Wenyewe wakataja tafsiri za uwongo hapa, na walipozifasiri khasa katika mahala pake wakasahau. Wakafasiri vile vile — kama wanavyofasiri wafasiri wengine — kwa kufa na kufufuka. Tazama Mwenyezi Mungu alivyowahizi.

57. Manna ni kitu kama asali kilichokuwa kinatoka katika miti waliyokuwa wakikutana nayo huko jangwani iwe ndiyo kama asali au haluwa kwao. Na Salwa ni ndege waliokuwa wakiwajia kwa wingi kabisa humo njiani, ili wawachinje wawale pamoja na haluwa hiyo. Ndege hao wakishabihi hawa ndege wanaoitwa 'tomboro'.

58. Mji huo (au nchi hizo) ni hii Sham. Waliambiwa wende wakakae nchi hiyo, badala ya Misr, na waingie kwa shuruti hizo; lakini hawakuzitekeleza.

59. Inasemekana kuwa adhabu yenyewe ilikuwa ni tauni na walikufa chungu ya watu kwa ugonjwa huo.

60. Na (kumbukeni khabari hii nayo)· Musa alipoomba maji kwa ajili ya watu wake, tukasema: "Lipige jiwe kwa fimbo yako;" Mara zikabubujika humo chemchem kumi na mbili; kila kabila ikajua mahali pake pa kunywea. (Tukawaambia:) Kuleni na kunyweni katika riziki ya Mwenyezi Mungu, wala msiasi katika ardhi mkafanya uharibifu.

وَإِذِ اسْتَسْقَىٰ مُوسَىٰ لِقَوْمِهِ فَقُلْنَا اضْرِب
بِّعَصَاكَ الْحَجَرَ ۖ فَانفَجَرَتْ مِنْهُ اثْنَتَا عَشْرَةَ عَيْنًا ۖ
قَدْ عَلِمَ كُلُّ أُنَاسٍ مَّشْرَبَهُمْ ۖ كُلُوا وَاشْرَبُوا مِن رِّزْقِ
اللَّهِ وَلَا تَعْثَوْا فِي الْأَرْضِ مُفْسِدِينَ ٦٠

61. Na (kumbukeni khabari hii kadhalika:) Mliposema: "Ewe Musa! Hatuwezi kusubiri kwa chakula cha namna moja tu, basi tuombee kwa Mola wako atutolee vile vinavyooteshwa na ardhi, kama mboga zake na matango yake na ngano yake (au thomu zake) na adesi zake na vitunguu vyake." Akasema (Mwenyezi Mungu): "Mnabadili vitu duni kwa vile vilivyo bora? Nendeni kwenye mji, huko mtapata mlivyoviomba"; Na ikapigwa juu yao (chapa ya) dhila (unyonge) na umasikini; nawakastahiki ghadhabu ya Mwenyezi Mungu: Na haya ni kwa sababu walikuwa wakiyakataa maneno ya Mwenyezi Mungu, na wakiwauwa Manabii pasipo haki. Basi haya ni kwa sababu ya kuasi kwao na kupindukia mipaka (ya Mwenyezi Mungu).

وَإِذْ قُلْتُمْ يَا مُوسَىٰ لَن نَّصْبِرَ عَلَىٰ طَعَامٍ وَاحِدٍ فَادْعُ
لَنَا رَبَّكَ يُخْرِجْ لَنَا مِمَّا تُنبِتُ الْأَرْضُ مِن بَقْلِهَا
وَقِثَّائِهَا وَفُومِهَا وَعَدَسِهَا وَبَصَلِهَا ۖ قَالَ أَتَسْتَبْدِلُونَ
الَّذِي هُوَ أَدْنَىٰ بِالَّذِي هُوَ خَيْرٌ ۚ اهْبِطُوا مِصْرًا فَإِنَّ
لَكُم مَّا سَأَلْتُمْ ۗ وَضُرِبَتْ عَلَيْهِمُ الذِّلَّةُ وَالْمَسْكَنَةُ
وَبَاءُوا بِغَضَبٍ مِّنَ اللَّهِ ۗ ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ كَانُوا يَكْفُرُونَ
بِآيَاتِ اللَّهِ وَيَقْتُلُونَ النَّبِيِّينَ بِغَيْرِ الْحَقِّ ۗ ذَٰلِكَ بِمَا
عَصَوا وَّكَانُوا يَعْتَدُونَ ٦١ ع

62. Katika walioamini (Mitume ya zamani huko) na Mayahudi na Wakristo na Wasabai; yo yote (miongoni mwao) atakayemwamini Mwenyezi Mungu (sasa kama anavyosema Nabii Muhammad) na akaamini siku ya mwisho na akafanya vitendo vizuri, basi watapata thawabu zao kwa Mola wao, wala haitakuwa khofu juu yao, wala hawatahuzunika.

إِنَّ الَّذِينَ آمَنُوا وَالَّذِينَ هَادُوا وَالنَّصَارَىٰ
وَالصَّابِئِينَ مَنْ آمَنَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَعَمِلَ
صَالِحًا فَلَهُمْ أَجْرُهُمْ عِندَ رَبِّهِمْ وَلَا خَوْفٌ
عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ٦٢

---

61. Muradi wa chakula cha namna moja ni ile Manna na Salwa. Hawataki tena. Sifa hii wanayo Mayahudi mpaka leo. Hapana historia iliyojaa malalamiko kama yao. Hili linakubaliwa na wataalamu wote wa historia.

Na katika maasia makubwa waliyofanya Mayahudi ni kuwaua Manabii wa Mwenyezi Mungu kama Zakaria (Zacharia) na Yahya (John); na wakataka kumwua Nabii Isa na Nabii Muhammad pia.

62. Muradi wa Aya hii ni kwamba jambo kubwa la kupatia mema na kuepuka khofu na huzuni za Siku ya Kiyama ni kumwamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho, na kufanya amali njema. Na hili halikuhusikana na Waislamu peke yao, bali linawakusanya watu wa dini zote zilizotajwa hapa. Makubwa katika mambo mema ni kufuata Amri za Mwenyezi Mungu zilizobainiwa katika vitabu vyake vitakatifu. Na miongoni mwa Amri zilizomo katika vitabu vya Mayahudi na Wakristo ni kumuamini Mtume mtukufu Muhammad s.a.w. Tazama Marejezo 18: 17-19 na Johana 14: 19-26.

Wamepachika katika maelezo ya Aya walioihisabu kuwa ni ya 63 maneno ya uwongo haya: "Tukumbuke ya kuwa Mtume s.a.w. pia alitabiri ya kuwa Uislamu utainuka tena katika kufika kwa Masihi Aliyeahidiwa. Kufika kwa Seyyidna Ahmad, mwanzo wa karne hii ya 14 ya Hijra . . ." Kwa nini wasikitaje kitabu hicho?

Uwongo kabisa: Hakuna Hadithi hii katika kitabu cho chote kile kinachotaja Hadithi za Mtume. Hata wao juu ya uzushi wao hawakujasirisha kukitaja kitabu hicho kisichokuwapo ulimwenguni. Basi, hamu yao Makadiyani wawapoteze Waislamu wawe makafiri. Kila wanayoyafanya, lengo lao ni kuwafanya Waislamu wawe makafiri.

63. Na (kumbukeni habari hii vile vile enyi Mayahudi): Tulipotwaa ahadi yenu (ahadi ya wazee wenu katika zama za Nabii Musa) na tukauinua mlima juu yenu (tukakwambieni): "Kamateni kwa nguvu haya tuliyokupeni na yakumbukeni yaliyomo ndani yake ili mpate kuwa wacha Mungu."

وَإِذْ أَخَذْنَا مِيثَاقَكُمْ وَرَفَعْنَا فَوْقَكُمُ الطُّورَ
خُذُوا مَا آتَيْنَاكُم بِقُوَّةٍ وَاذْكُرُوا مَا فِيهِ
لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ ﴿٦٣﴾

64. Kisha mlikengeuka (mligeuka) baada ya haya. Na lau kuwa si fadhila za Mwenyezi Mungu juu yenu na rehema Zake, mngalikuwa miongoni mwa wenye kukhasirika (daima).

ثُمَّ تَوَلَّيْتُم مِّن بَعْدِ ذَٰلِكَ ۖ فَلَوْلَا فَضْلُ اللَّهِ
عَلَيْكُمْ وَرَحْمَتُهُ لَكُنتُم مِّنَ الْخَاسِرِينَ ﴿٦٤﴾

65. Na kwa yakini mmekwisha kujua (khabari za) wale walioasi miongoni mwenu katika (amri ya kuihishimu) Jumaamosi. Basi Tukawaambia: "Kuweni manyani wadhalilifu."

وَلَقَدْ عَلِمْتُمُ الَّذِينَ اعْتَدَوْا مِنكُمْ فِي
السَّبْتِ فَقُلْنَا لَهُمْ كُونُوا قِرَدَةً خَاسِئِينَ ﴿٦٥﴾

66. Kwa hivyo tukaifanya (adhabu hiyo) kuwa onyo kwa wale waliokuwa katika zama zao na waliokuja nyuma yao, na (tukaifanya ni) mauidha kwa wamchao Mwenyezi Mungu.

فَجَعَلْنَاهَا نَكَالًا لِّمَا بَيْنَ يَدَيْهَا وَمَا خَلْفَهَا
وَمَوْعِظَةً لِّلْمُتَّقِينَ ﴿٦٦﴾

67. Na (kumbukeni khabari hii pia enyi Mayahudi:) Musa alipowaambia watu wake: "Hakika Mwenyezi Mungu anakuamrisheni mchinje ng'ombe." Wakasema: "Je ! Unatufanyia mzaha (sasa)?" Akasema: "(La!) Najikinga kwa Mwenyezi Mungu kuwa miongoni mwa wajinga (wanaofanya mizaha katika mambo ya dini)."

وَإِذْ قَالَ مُوسَىٰ لِقَوْمِهِ إِنَّ اللَّهَ يَأْمُرُكُمْ أَن تَذْبَحُوا
بَقَرَةً ۖ قَالُوا أَتَتَّخِذُنَا هُزُوًا ۖ قَالَ أَعُوذُ بِاللَّهِ
أَنْ أَكُونَ مِنَ الْجَاهِلِينَ ﴿٦٧﴾

---

63. Mayahudi walipopewa ile *Taurati* walifanya ukaidi kuipokea. Mwenyezi Mungu akaliamrisha jabali lililokuwa limezunguka mji ule linyanyuke juu liwafunike kama kiwingu; likanyanyuka namna hivyo, liko juu ya tosi zao. Na wakaambiwa: "Kama hamtafuata, litakuangukieni likusagenisageni." Hapo ndipo walipofuata; kisha wakatupilia mbali.

Na hayo maelezo waliyoyatoa Makadiyani katika Aya walizozifanya ni za 64 na 66 wako wanavyuoni wachache kabisa waliosema hivyo. Basi kuitakidi hivyo si ukafiri.

65. Mayahudi walikatazwa katika dini yao kufanya kazi siku ya Jumaamosi—wawemo ibadani tu. Lakini baadhi yao waliasi, ima kwa ujanja au kinagaubaga (dhahiri bila ya kudanganya kwa kufanya ujanja wo wote). Basi Mwenyezi Mungu aliwaadhibu wote waliokhalifu, hata waliokhalifu kwa ujanjaujanja.

Miongoni mwa hao waliokhalifu kwa ujanja ni wavuvi wa samaki. Walikuwa wakiweka madema yao na kutega mazio yao laasiri ya Ijumaa, ili wanase Jumaamosi ili isipite bure siku hiyo ya Jumaamosi; iwe wameipatia fa'ida ya kilimwenguni japo kuwa wamekatazwa. Basi wakenda wakiwachukua Jumaapili. Mwenyezi Mungu akawatia adabu hii iliyotajwa katika Aya hii.

Basi na hao wanaodhulumu mali za watu kwa jina la 'Bayilkat-i' . . . na kwa njia nyingine za udanganyifu, wanangojwa na adhabu kubwa kabisa ya Mwenyezi Mungu. Baadhi ya wanavyuoni wanasema kuwa si lazima kuwa Mayahudi hao waligeuzwa manyani kwa sura. Inawezekana kuwa walipewa sifa za manyani tu, kama unyonge wa daima, ukosefu wa ilimu, kufanya kila wanalolipenda japo halikubaliwi na akili, na kama hayo katika sifa za manyani.

67. Mtu mmoja katika zama za Nabii Musa aliuawa, asijulikane aliyemuua. Akaja akaulizwa Nabii Musa. Mwenyezi Mungu akamletea Wahyi awambie wachinje ng'ombe, kisha watwae mkia wa ng'ombe huyo, wamchape huyo maiti; atafufuka amtaje huyo aliyemuua, apate kulipwa kisasi chake. Au akisha kuchinjwa waje watu wanaotuhumiwa washikishwe ng'ombe huyo (kama kiapo). Atakayefazaika abanwe mpaka abainishe aliyeua. Na pengine atakiri kuwa yeye ndiye aliyeua.

Nabii Musa alipowajuvya khabari hii waliona kuwa wanarushwa tu. Basi wakashadidishashadidisha. Na Mungu akawashadidishia. Hata walipompata wa namna hiyo wakamchinja, taabu nyingi zilikuwa zimekwishawafika na mali mengi yamekwishapotea.

68. Wakasema: "Tuombee kwa Mola wako atupambanulie ni (wa umri) gani (ng'ombe huyo)?" Akasema: "Hakika Yeye anasema kwamba ng'ombe huyo si mzee wala si mchanga, bali ni wa katikati baina ya hao. Basi fanyeni mnavyoamrishwa."

قَالُوا ادْعُ لَنَا رَبَّكَ يُبَيِّن لَّنَا مَا هِيَ ۚ قَالَ إِنَّهُ يَقُولُ
إِنَّهَا بَقَرَةٌ لَّا فَارِضٌ وَلَا بِكْرٌ عَوَانٌ بَيْنَ ذَٰلِكَ
فَافْعَلُوا مَا تُؤْمَرُونَ ﴿٦٨﴾

69. Wakasema: "Tuombee kwa Mola wako atupambanulie nini rangi yake." Akasema: "Yeye anasema, kuwa ng'ombe huyo ni wa manjano, na rangi yake imewiva sana, huwapendeza wanaomtazama."

قَالُوا ادْعُ لَنَا رَبَّكَ يُبَيِّن لَّنَا مَا لَوْنُهَا ۚ قَالَ إِنَّهُ
يَقُولُ إِنَّهَا بَقَرَةٌ صَفْرَاءُ فَاقِعٌ لَّوْنُهَا تَسُرُّ
النَّاظِرِينَ ﴿٦٩﴾

70. Wakasema: "Tuombee kwa Mola wako atupambanulie ni vipi hali yake; hakika ng'ombe (waliotajwa kwa sifa hizo) wanafanana; (basi yupi)? Na kwa yakini kama Mungu akipenda (tutafuata) tuwe wenye kuongoka."

قَالُوا ادْعُ لَنَا رَبَّكَ يُبَيِّن لَّنَا مَا هِيَ إِنَّ الْبَقَرَ تَشَابَهَ
عَلَيْنَا وَإِنَّا إِن شَاءَ اللَّهُ لَمُهْتَدُونَ ﴿٧٠﴾

71. Akasema: "Yeye anasema: Kuwa huyo si ng'ombe aliyetiwa kazini kulima ardhi wala kutilia maji mimea, safi kabisa rangi yake, hana kipaku ndani yake." Wakasema: "Sasa umeleta (maneno ya) haki." Basi wakamchinja, na walikuwa mbali na kufanya hayo.

قَالَ إِنَّهُ يَقُولُ إِنَّهَا بَقَرَةٌ لَّا ذَلُولٌ تُثِيرُ الْأَرْضَ
وَلَا تَسْقِي الْحَرْثَ مُسَلَّمَةٌ لَّا شِيَةَ فِيهَا ۚ قَالُوا
الْآنَ جِئْتَ بِالْحَقِّ ۚ فَذَبَحُوهَا وَمَا كَادُوا يَفْعَلُونَ ﴿٧١﴾ ع

72. Na (kumbukeni khabari hii inayotajwa sasa hivi:) Mlipoiua nafsi, kisha mkakhitilafiana kwa hayo; (wengine wanasema kauawa na Fulani na wengine wanasema Fulani mwingine). Na Mwenyezi Mungu ni Mtoaji wa hayo mliyokuwa mkiyaficha. (Basi akayatoa akajulikana huyo aliyemwua).

وَإِذْ قَتَلْتُمْ نَفْسًا فَادَّارَأْتُمْ فِيهَا ۖ وَاللَّهُ مُخْرِجٌ
مَّا كُنتُمْ تَكْتُمُونَ ﴿٧٢﴾

73. Tukasema: "Mpigeni kwa baadhi (sehemu) yake (huyu ng'ombe)." Ndivyo hivi Mwenyezi Mungu huwahuisha wafu; na anakuonyesheni Dalili zake ili mpate kufahamu.

فَقُلْنَا اضْرِبُوهُ بِبَعْضِهَا ۚ كَذَٰلِكَ يُحْيِي اللَّهُ الْمَوْتَىٰ
وَيُرِيكُمْ آيَاتِهِ لَعَلَّكُمْ تَعْقِلُونَ ﴿٧٣﴾

74. Kisha nyoyo zenu zikawa ngumu baada ya hayo (yote); hata zikawa kama mawe au ngumu zaidi; kwani kuna mawe mengine yanayobubujika mito ndani yake, na kuna mengine yanayopasuka yakatoka maji ndani yake; na kuna mengine huanguka kwa sababu ya khofu ya Mwenyezi Mungu. (Na nyinyi Mayahudi hamuathiriki kwa lo lote). Na Mwenyezi Mungu si Mwenye kughafilika na mnayoyafanya.

ثُمَّ قَسَتْ قُلُوبُكُم مِّن بَعْدِ ذَٰلِكَ فَهِيَ
كَالْحِجَارَةِ أَوْ أَشَدُّ قَسْوَةً ۚ وَإِنَّ مِنَ الْحِجَارَةِ لَمَا
يَتَفَجَّرُ مِنْهُ الْأَنْهَارُ ۚ وَإِنَّ مِنْهَا لَمَا يَشَّقَّقُ فَيَخْرُجُ
مِنْهُ الْمَاءُ ۚ وَإِنَّ مِنْهَا لَمَا يَهْبِطُ مِنْ خَشْيَةِ اللَّهِ ۗ
وَمَا اللَّهُ بِغَافِلٍ عَمَّا تَعْمَلُونَ ﴿٧٤﴾

---

72. Huu ndio mwanzo wa kisa cha Ng'ombe. Ukisoma vitabu vya watu mafasihi leo utaona wakitoa kisa hawaanzi mwanzo, bali huanzia kati au mwisho. Basi msemo wa namna hii umeanza kutumika katika Quran.

74. Mawe pamoja na ugumu wake hupasuka yakatoka maji, na pamoja na kuwa hayana akili hayakhalifu amri ya Mungu. Lakini Mayahudi hawaathiriki kwa waadhi, pamoja na kupewa akili na kupelekewa Mitume na Vitabu na kuonyeshwa miujiza kadha wa kadha.

75. Mnatumaini (nyinyi Waislamu) ya kwamba watakuaminini (hao Mayahudi); na hali baadhi yao walikuwa wanasikia maneno ya Mwenyezi Mungu, kisha wanayabadili baada ya kuwa wameyafahamu; na hali wanajua?

أَفَتَطْمَعُونَ أَن يُؤْمِنُوا لَكُمْ وَقَدْ كَانَ فَرِيقٌ
مِّنْهُمْ يَسْمَعُونَ كَلَامَ اللَّهِ ثُمَّ يُحَرِّفُونَهُ مِن بَعْدِ
مَا عَقَلُوهُ وَهُمْ يَعْلَمُونَ ٧٥

76. Na wanapokutana na wale walioamini husema: "Tumeamini (kuwa kweli huyu Nabii Muhammad Mtume wa haki, katajwa katika vitabu vyetu)." Na wanapokuwa peke yao, wao kwa wao, husema: "Mnawaambia (Waislamu) aliyokufungulieni Mwenyezi Mungu ili wapate kukuhojini mbele ya Mola wenu (kwa yaliyo katika vitabu vya Mola wenu vilivyo kwenu) (wakuhojini kwa kitabu kinachotoka kwa Mola wenu)? Hamna akili?

وَإِذَا لَقُوا الَّذِينَ آمَنُوا قَالُوا آمَنَّا وَإِذَا خَلَا
بَعْضُهُمْ إِلَىٰ بَعْضٍ قَالُوا أَتُحَدِّثُونَهُم بِمَا فَتَحَ اللَّهُ
عَلَيْكُمْ لِيُحَاجُّوكُم بِهِ عِندَ رَبِّكُمْ
أَفَلَا تَعْقِلُونَ ٧٦

77. (Mwenyezi Mungu anasema:) Hawajui ya kwamba Mwenyezi Mungu anayajua wanayoyaficha na wanayoyadhihirisha?

أَوَلَا يَعْلَمُونَ أَنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ مَا يُسِرُّونَ
وَمَا يُعْلِنُونَ ٧٧

78. Na wako miongoni mwao (hao Mayahudi) watu wasiojua kusoma; hawajui (kusoma na kufahamu) Kitabu (cha Mwenyezi Mungu; hawajui) isipokuwa tamaa tu za upuuzi, nao hawana ila kudhani tu.

وَمِنْهُمْ أُمِّيُّونَ لَا يَعْلَمُونَ الْكِتَابَ إِلَّا أَمَانِيَّ وَإِنْ
هُمْ إِلَّا يَظُنُّونَ ٧٨

79. Basi adhabu kali itawathibitikia wanaoandika kitabu kwa mikono yao, kisha wakasema: "Hiki kimetoka kwa Mwenyezi Mungu." (Wanasema uwongo huo) Ili wachukue thamani ndogo ya kilimwengu. Basi ole wao kwa yale waliyoyaandika kwa mikono yao (wakasingizia kuwa ya Mungu). Na ole wao kwa yale wanayoyachuma.

فَوَيْلٌ لِّلَّذِينَ يَكْتُبُونَ الْكِتَابَ بِأَيْدِيهِمْ ثُمَّ يَقُولُونَ
هَٰذَا مِنْ عِندِ اللَّهِ لِيَشْتَرُوا بِهِ ثَمَنًا قَلِيلًا فَوَيْلٌ لَّهُم
مِّمَّا كَتَبَتْ أَيْدِيهِمْ وَوَيْلٌ لَّهُم مِّمَّا يَكْسِبُونَ ٧٩

80. Na walisema: "Hautatugusa Moto (wa Jahannam) isipokuwa kwa siku chache tu." Sema: "Je! Mmepata ahadi kwa Mwenyezi Mungu? Kwa hivyo hatakhalifu ahadi yake. Au mnamsingizia Mwenyezi Mungu mambo msiyoyajua."

وَقَالُوا لَن تَمَسَّنَا النَّارُ إِلَّا أَيَّامًا مَّعْدُودَةً قُلْ أَتَّخَذْتُمْ
عِندَ اللَّهِ عَهْدًا فَلَن يُخْلِفَ اللَّهُ عَهْدَهُ أَمْ تَقُولُونَ
عَلَى اللَّهِ مَا لَا تَعْلَمُونَ ٨٠

---

75. Kwa kuwa Mayahudi ni watu wa kitabu *(Taurati)* ambacho kimetaja sifa ya Nabii Muhammad s.a.w., Mtume alikuwa akitaraji sana kuwa watamuamini na kumfuata. Kwa Aya hii Mwenyezi Mungu Anawatoa tamaa Mtume na Masahaba wake wasitaraji kuwa Mayahudi wataamini, pamoja na kuwaonesha kuwa wao wametangulia kufanya Makubwa zaidi ya hayo: yaani kubadilisha maneno ya Mwenyezi Mungu.

Mayahudi wamebadilisha maneno ya *Taurati* kwa kuondosha matamko na kutia mengine, kwa kugeuza tafsiri, kwa kupunguza na kwa kuongeza pia.

76. Mayahudi walipokuwa wakimnafikia Mtume s.a.w. na wafuasi wake na wakiwakubalia kuwa kweli Mtume Muhammad s.a.w. katajwa katika *Taurati*, wenzao walikuwa wakiwalaumu kwa kule kuwafunulia Waislamu mambo ambayo Mayahudi wamewafikiana kuwa wayafiche. Basi Mwenyezi Mungu Anawajibu kwa Aya ifuwatayo kwamba Yeye Anayajuwa wanayoyaficha na wanayoyadhihirisha.

80-82. Mayahudi, kwa kujitapa kuwa ni watukufu, kwa kule kunasibikana kwao na Mitume, walikuwa wakidai kuwa hawataadhibiwa illa siku arubaini tu ambazo wazee wao waliabudu ndama. Mwenyezi Mungu Anawakadhibisha kwa Aya hizi kwamba yo yote atakayefanya maovu ataadhibiwa kwa maovu yake; na hapana litakalomnusuru mtu ila imani na amali njema.

81. Naam, wanaochuma ubaya — na makosa yao yakawazunguka — hao ndio watu wa Motoni; humo watakaa milele.

بَلَىٰ مَن كَسَبَ سَيِّئَةً وَأَحَاطَتْ بِهِۦ خَطِيٓـَٔتُهُۥ فَأُولَٰٓئِكَ
أَصْحَٰبُ ٱلنَّارِ هُمْ فِيهَا خَٰلِدُونَ ﴿٨١﴾

82. Na wale walioamini na kutenda mema, hao ndio watu wa Peponi, humo watakaa milele.

وَٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ وَعَمِلُوا۟ ٱلصَّٰلِحَٰتِ أُولَٰٓئِكَ أَصْحَٰبُ
ٱلْجَنَّةِ هُمْ فِيهَا خَٰلِدُونَ ﴿٨٢﴾

83. Na (kumbukeni khabari hii:) Tulipochukua ahadi ya kizazi cha Israili (Mayahudi tukawaambia) kuwa "Hamtamwabudu yo yote (sasa) ila Mwenyezi Mungu; na muwafanyie wema wazazi na jamaa na mayatima na masikini, na semeni na watu kwa wema na simamisheni Sala na toeni Zaka." Kisha mkageuka isipokuwa wachache tu katika nyinyi na (hivi sasa pia) nyinyi mnapuuza (hivi).

وَإِذْ أَخَذْنَا مِيثَٰقَ بَنِىٓ إِسْرَٰٓءِيلَ لَا تَعْبُدُونَ إِلَّا
ٱللَّهَ وَبِٱلْوَٰلِدَيْنِ إِحْسَانًا وَذِى ٱلْقُرْبَىٰ وَٱلْيَتَٰمَىٰ
وَٱلْمَسَٰكِينِ وَقُولُوا۟ لِلنَّاسِ حُسْنًا وَأَقِيمُوا۟ ٱلصَّلَوٰةَ
وَءَاتُوا۟ ٱلزَّكَوٰةَ ثُمَّ تَوَلَّيْتُمْ إِلَّا قَلِيلًا مِّنكُمْ وَأَنتُم
مُّعْرِضُونَ ﴿٨٣﴾

84. Na (kumbukeni khabari hii nayo:) Tulipochukua ahadi yenu; kuwa hamtamwaga damu zenu, wala hamtawatoa watu wenu katika miji yenu; nanyi mkakubali (wala msifuate). Na mnajua (kuwa mlikubali wala msifuate).

وَإِذْ أَخَذْنَا مِيثَٰقَكُمْ لَا تَسْفِكُونَ دِمَآءَكُمْ وَلَا تُخْرِجُونَ
أَنفُسَكُم مِّن دِيَٰرِكُمْ ثُمَّ أَقْرَرْتُمْ وَأَنتُمْ تَشْهَدُونَ ﴿٨٤﴾

85. Kisha nyinyi mnawaua watu wenu, na mnawatoa baadhi yenu katika nyumba zao; mnasaidiana juu yao (katika kuwadhuru) kwa (njia za kukupatisheni) dhambi na (kuonyesha) uadui. Na wakikujieni mateka mnawakomboa, na hali imeharimishwa kwenu kuwatoa. Je! Mnaamini baadhi ya Kitabu na kukataa baadhi (yake)? Basi hakuna malipo kwa mwenye kufanya haya katika nyinyi ila fedheha katika maisha ya dunia; na siku ya Kiyama watapelekwa katika adhabu kali. Na Mwenyezi Mungu si mwenye kughafilika na yale mnayoyatenda.

ثُمَّ أَنتُمْ هَٰٓؤُلَآءِ تَقْتُلُونَ أَنفُسَكُمْ وَتُخْرِجُونَ فَرِيقًا
مِّنكُم مِّن دِيَٰرِهِمْ تَظَٰهَرُونَ عَلَيْهِم بِٱلْإِثْمِ
وَٱلْعُدْوَٰنِ وَإِن يَأْتُوكُمْ أُسَٰرَىٰ تُفَٰدُوهُمْ وَهُوَ
مُحَرَّمٌ عَلَيْكُمْ إِخْرَاجُهُمْ أَفَتُؤْمِنُونَ بِبَعْضِ ٱلْكِتَٰبِ
وَتَكْفُرُونَ بِبَعْضٍ فَمَا جَزَآءُ مَن يَفْعَلُ ذَٰلِكَ
مِنكُمْ إِلَّا خِزْىٌ فِى ٱلْحَيَوٰةِ ٱلدُّنْيَا وَيَوْمَ ٱلْقِيَٰمَةِ
يُرَدُّونَ إِلَىٰٓ أَشَدِّ ٱلْعَذَابِ وَمَا ٱللَّهُ بِغَٰفِلٍ
عَمَّا تَعْمَلُونَ ﴿٨٥﴾

86. Hao ndio waliokhiari (starehe za) uhai wa dunia badala ya (starehe za) Akhera; kwa hivyo hawatapunguziwa adhabu wala hawatanusuriwa.

أُولَٰٓئِكَ ٱلَّذِينَ ٱشْتَرَوُا۟ ٱلْحَيَوٰةَ ٱلدُّنْيَا بِٱلْءَاخِرَةِ
فَلَا يُخَفَّفُ عَنْهُمُ ٱلْعَذَابُ وَلَا هُمْ يُنصَرُونَ ﴿٨٦﴾

87. Na hakika tulimpa Musa Kitabu na

وَلَقَدْ ءَاتَيْنَا مُوسَى ٱلْكِتَٰبَ وَقَفَّيْنَا مِنۢ بَعْدِهِۦ

---

Basi tunawanasihi wale wanaojigamba kwa nasabu na kuona kuwa nasabu zao zitawatosha Mbele ya Mwenyezi Mungu. Mungu ameyakataa haya katika mahala pengi katika Qurani. Pamoja katika humo ni aya ya 101 ya Suratul Muuminuun, na Mtume ameyakataa kwa hadithi nyingi na tazama maelezo ya aya ya 124 ya sura hii hii.

85. Madina kulikuwa na makabila mawili: Aws na Khazraj. Watu wa makabila haya kabla ya kusilimu walikuwa mara kwa mara wakipigana. Mayahudi wa Madina waligawanyika mafungu mawili, wengine wakaunga upande wa Aws na wengine upande wa Khazraj. Kwa hivyo wakati yanapopigana makabila mawili haya, Mayahudi wa upande mmoja walikuwa wakiua Mayahudi wenzao wa upande mwengine. Na iwapo baadhi ya jamaa zao wamekuwa mateka, walikuwa wakiwakomboa. Hapa wanaambiwa "Iwapo mnawakomboa mateka wa Kiyahudi kwa sababu ya kufuata Taurati, kwa nini mnapigana nyinyi kwa nyinyi, na hilo pia limekatazwa katika Taurati? Mnaamini baadhi ya Taurati na kuikanusha baadhi nyingine?"

Na kama Alivyosema Mwenyezi Mungu: walipata fedheha ya kuuliwa, kutolewa katika miji na kufanywa mateka. Na Siku ya Kiyama watapata adhabu iliyotajwa mwisho wa Aya.

87. Kwa Waislamu "Roho mtakatifu" ni Malaika Jibril, si yule wanaedai Wakristo kuwa ni mmoja wa asli ya

بِالرُّسُلِ ۖ وَآتَيْنَا عِيسَى ابْنَ مَرْيَمَ الْبَيِّنَاتِ
وَأَيَّدْنَاهُ بِرُوحِ الْقُدُسِ ۗ أَفَكُلَّمَا جَاءَكُمْ
رَسُولٌ بِمَا لَا تَهْوَىٰ أَنْفُسُكُمُ اسْتَكْبَرْتُمْ فَفَرِيقًا
كَذَّبْتُمْ وَفَرِيقًا تَقْتُلُونَ ﴿٨٧﴾

tukawafuatisha Mitume (wengine) baada yake. na tukampa Isa, mwana wa Mariamu, hoja zilizo waziwazi, na tukamtia nguvu kwa Roho mtakatifu (Jibril). Basi (nyinyi Mayahudi kazi yenu ndiyo hii tu:) Kila walipokufikieni Mitume kwa yale yasiyoyapenda nafsi zenu, mlijivuna, kundi moja mkalikadhibisha na kundi (jingine) mkaliua!

وَقَالُوا قُلُوبُنَا غُلْفٌ ۚ بَلْ لَعَنَهُمُ اللَّهُ
بِكُفْرِهِمْ فَقَلِيلًا مَا يُؤْمِنُونَ ﴿٨٨﴾

88. Na walisema (alipokuja Nabii Muhammad akawafundisha dini:) "Nyoyo zetu zimefunikwa (hatufahamu unayoyasema)." (Nao ni waongo katika majidai hayo). Bali Mwenyezi Mungu amewalaani kwa kufuru zao; kwa hivyo ni kidogo tu wanayoyaamini.

وَلَمَّا جَاءَهُمْ كِتَابٌ مِنْ عِنْدِ اللَّهِ مُصَدِّقٌ لِمَا
مَعَهُمْ وَكَانُوا مِنْ قَبْلُ يَسْتَفْتِحُونَ عَلَى الَّذِينَ كَفَرُوا
فَلَمَّا جَاءَهُمْ مَا عَرَفُوا كَفَرُوا بِهِ ۚ فَلَعْنَةُ اللَّهِ
عَلَى الْكَافِرِينَ ﴿٨٩﴾

89. Na kilipowafikia (wakati wa Nabii Muhammad hiki) Kitabu kitokacho kwa Mwenyezi Mungu kisadikishacho yaliyo pamoja nao (walikadhibisha); na zamani walikuwa wakiwafungulia makafiri (khabari ya Mtume huyo). Lakini yalipowafikia yale waliyokuwa wakiyajua waliyakataa. Basi laana ya Mwenyezi Mungu iko juu ya makafiri (hao).

بِئْسَمَا اشْتَرَوْا بِهِ أَنْفُسَهُمْ أَنْ يَكْفُرُوا بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ
بَغْيًا أَنْ يُنَزِّلَ اللَّهُ مِنْ فَضْلِهِ عَلَىٰ مَنْ يَشَاءُ
مِنْ عِبَادِهِ ۖ فَبَاءُوا بِغَضَبٍ عَلَىٰ غَضَبٍ ۚ
وَلِلْكَافِرِينَ عَذَابٌ مُهِينٌ ﴿٩٠﴾

90. Kibaya kabisa walichouzia (starehe za) nafsi zao (za Akhera) ni kule kukataa aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu. (Wanakanusha hivyo) kwa ajili ya kuona maya (husuda) kwa kuwa Mwenyezi Mungu kawateremshia fadhila Zake awatakao katika waja Wake (wasiokuwa Mayahudi). Kwa hiyo wakastahiki (kwa Mwenyezi Mungu) ghadhabu (tena safari hii kwa kumkataa Nabii Muhammad) juu ya ghadhabu (juu ya ghadhabu walizoghadhibikiwa kwa kuwapinga hao Mitume waliotangulia); na watakuwa nayo makafiri (hao) adhabu ya kudhalilisha.

وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ آمِنُوا بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ قَالُوا نُؤْمِنُ بِمَا
أُنْزِلَ عَلَيْنَا وَيَكْفُرُونَ بِمَا وَرَاءَهُ ۚ وَهُوَ الْحَقُّ
مُصَدِّقًا لِمَا مَعَهُمْ ۗ قُلْ فَلِمَ تَقْتُلُونَ أَنْبِيَاءَ اللَّهِ
مِنْ قَبْلُ إِنْ كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ ﴿٩١﴾

91. Na wanapoambiwa (hao Mayahudi): "Yaaminini aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu," (kwa Nabii Muhammad) husema: "Tunaamini yaliyoteremshwa juu yetu (kwa Nabii Musa)"; na huyakataa yasiyokuwa hayo. Na hali ya kuwa hii (Quran) ndiyo haki inayosadikisha yale yaliyo pamoja nao. Sema: "Mbona mliwaua Mitume wa Mwenyezi Mungu hapo zamani kama mlikuwa mkiamini?"

---

Utatu (trinity).

Katika maelezo ya Aya walioifanya kuwa ni ya 88 Makadiyani wamepachika hivi "Kama Nabii yo yote akifika tumpime kwa juu ya mizani hii, je mambo anayoleta yanafurahikiwa sana na watu au yanakasirikiwa." Wamepachika haya wampe Utume huyo Mirza Ghulam wao. Na sisi tumekwisha kubainisha dhahir shahir. tuliporejeza maelezo ya kwenye Aya ya 4 *Suratul Baqarah* waliyoifanya Aya ya 5. Rejelea tulivyoyasema uzidi kuona uwongo wao na upotofu wao.

89. Kabla ya kuja Mtume Muhammad s.a.w. Mayahudi walikuwa wakiwapa khabari Waarabu kuwa karibuni

92. "Na alikufikieni Musa na hoja zilizo waziwazi, kisha mkamfanya ndama (kuwa mungu) baada yake (baada ya kuondoka kwake), na mkawa madhalimu (wa nafsi zenu)."

وَلَقَدْ جَآءَكُم مُّوسَىٰ بِالْبَيِّنَٰتِ ثُمَّ اتَّخَذْتُمُ الْعِجْلَ
مِنۢ بَعْدِهِۦ وَأَنتُمْ ظَٰلِمُونَ ﴿٩٢﴾

93. Na (kumbukeni khabari hii kadhalika:) Tulipochukua ahadi yenu (wazee wenu) na tukauinua mlima juu yenu (tukakwambieni): "Kamateni kwa nguvu haya tuliyokupeni na sikilizeni." Wakasema: "Tunasikia na tunakataa." Na wakanyweshwa nyoyoni mwao (mapenzi ya kuabudu) ndama kwa kufuru yao. Sema: "Ni kibaya kabisa (kitendo hicho) kilichokuamrishieni imani yenu; mkiwa ni wenye kuamini."

وَإِذْ أَخَذْنَا مِيثَٰقَكُمْ وَرَفَعْنَا فَوْقَكُمُ الطُّورَ ۖ
خُذُوا۟ مَآ ءَاتَيْنَٰكُم بِقُوَّةٍ وَاسْمَعُوا۟ ۖ قَالُوا۟ سَمِعْنَا
وَعَصَيْنَا وَأُشْرِبُوا۟ فِى قُلُوبِهِمُ الْعِجْلَ بِكُفْرِهِمْ ۚ
قُلْ بِئْسَمَا يَأْمُرُكُم بِهِۦٓ إِيمَٰنُكُمْ إِن كُنتُم مُّؤْمِنِينَ ﴿٩٣﴾

94. Sema (kuwaambia Mayahudi): "Ikiwa nyumba ya Akhera hiyo iliyoko kwa Mwenyezi Mungu ni yenu nyinyi tu bila ya watu wengine (kama mnavyosema); basi tamanini mauti kama nyinyi ni wasema kweli". (Atakayesema: "Natamani kufa" atakufa sasa hivi. Basi wakakataa kutamani huko).

قُلْ إِن كَانَتْ لَكُمُ الدَّارُ الْءَاخِرَةُ عِندَ اللَّهِ خَالِصَةً
مِّن دُونِ النَّاسِ فَتَمَنَّوُا۟ الْمَوْتَ إِن كُنتُمْ صَٰدِقِينَ ﴿٩٤﴾

95. Wala hawatayatamani kabisa kwa sababu ya yale ambayo mikono yao imeyafanya; na Mwenyezi Mungu anawajua vyema madhalimu.

وَلَن يَتَمَنَّوْهُ أَبَدًۢا بِمَا قَدَّمَتْ أَيْدِيهِمْ ۗ وَاللَّهُ عَلِيمٌۢ
بِالظَّٰلِمِينَ ﴿٩٥﴾

96. Na utawaona (Mayahudi) wana hamu kubwa ya kuishi kuliko watu wengine, na kuliko wale wamshirikishao Mungu (wasioamini Akhera); kila mmoja katika wao anapenda apewe umri wa miaka elfu. Na huko kupewa kwake umri mwingi hakuwezi kumwondoshea adhabu; na Mwenyezi Mungu anayaona (yote) wanayoyafanya.

وَلَتَجِدَنَّهُمْ أَحْرَصَ النَّاسِ عَلَىٰ حَيَوٰةٍ ۛ وَمِنَ
الَّذِينَ أَشْرَكُوا۟ ۛ يَوَدُّ أَحَدُهُمْ لَوْ يُعَمَّرُ أَلْفَ سَنَةٍ
وَمَا هُوَ بِمُزَحْزِحِهِۦ مِنَ الْعَذَابِ أَن يُعَمَّرَ ۗ
وَاللَّهُ بَصِيرٌۢ بِمَا يَعْمَلُونَ ﴿٩٦﴾

97. Sema: "Anayemfanyia ushinde Jibril (kwa kuwa ndiye aliyemletea Utume Nabii Muhammad asiwapelekee Mayahudi) (ni bure, hana kosa Jibril); hakika yeye ameiteremsha Quran moyoni mwako kwa idhini ya Mwenyezi Mungu (sio kafanya kwa kupendelea kwake); (Quran) inayosadikisha yale yaliyokuwa kabla yake, na ni uwongozi na khabari njema kwa wanaoamini.

قُلْ مَن كَانَ عَدُوًّا لِّجِبْرِيلَ فَإِنَّهُۥ نَزَّلَهُۥ عَلَىٰ
قَلْبِكَ بِإِذْنِ اللَّهِ مُصَدِّقًا لِّمَا بَيْنَ يَدَيْهِ وَهُدًى
وَبُشْرَىٰ لِلْمُؤْمِنِينَ ﴿٩٧﴾

98. Anayemfanyia ushinde Mwenyezi Mungu na Malaika wake na Mitume wake na Jibril na Mikail, (anatafuta kuangamia) kwani Mwenyezi Mungu atakuwa mshinde wa makafiri hao.

مَن كَانَ عَدُوًّا لِّلَّهِ وَمَلَٰٓئِكَتِهِۦ وَرُسُلِهِۦ وَجِبْرِيلَ
وَمِيكَىٰلَ فَإِنَّ اللَّهَ عَدُوٌّ لِّلْكَٰفِرِينَ ﴿٩٨﴾

---

atadhihiria Mtume. Tazama Marejezo 18: 15-19 na Johana 1:25.

Ama kusema kuwa hao Mayahudi walikuwa wakiomba kwa jaha ya Mtume na wakishinda maadui zao-kuwa ndiyo muradi wa Aya hii-maneno haya hawakuyasema wale Wafasiri wa mwanzo kabisa (Salaf) wenye kutegemewa, kama Imam Ibn Jarir. Tazama kwenye Juzuu ya pili ya tafsiri yake-iliyosherehewa na kina Shakir-tangu sahifa 332 mpaka 335-hutaiona tafsiri hiyo. Wala hawakuitaja vile vile wale Wafasiri wanaotegemea Hadithi

99. Hakika tumekuteremshia hoja zilizo wazi; na hakuna wanaozikataa ila wale wanaovunja amri (za Mwenyezi Mungu).

وَلَقَدْ أَنزَلْنَا إِلَيْكَ آيَاتٍ بَيِّنَاتٍ ۖ
وَمَا يَكْفُرُ بِهَا إِلَّا الْفَاسِقُونَ ﴿٩٩﴾

100. Oh, kila mara wanapofunga ahadi (hawa Mayahudi), baadhi yao wanaitupa? Bali wengi katika wao hawaamini (lo lote).

أَوَكُلَّمَا عَاهَدُوا عَهْدًا نَّبَذَهُ فَرِيقٌ مِّنْهُم ۚ
بَلْ أَكْثَرُهُمْ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿١٠٠﴾

101. Na walipojiwa (Mayahudi) na Mtume kutoka kwa Mwenyezi Mungu, mwenye kusadikisha yale yaliyo pamoja nao, (Naye ni Nabii Muhammad), kundi moja miongoni mwa wale waliopewa Kitabu (cha Mwenyezi Mungu — Taurati) lilitupa Kitabu cha Mwenyezi Mungu (hicho) nyuma ya migongo yao kama kwamba hawajui.

وَلَمَّا جَاءَهُمْ رَسُولٌ مِّنْ عِندِ اللَّهِ مُصَدِّقٌ لِّمَا
مَعَهُمْ نَبَذَ فَرِيقٌ مِّنَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ
كِتَابَ اللَّهِ وَرَاءَ ظُهُورِهِمْ كَأَنَّهُمْ لَا يَعْلَمُونَ ﴿١٠١﴾

102. Wakafuata yale waliyoyafuata mashetani, (wakadai kuwa yalikuwa) katika ufalme wa (Nabii) Suleiman; na Suleiman hakukufuru, bali mashetani ndio waliokufuru, wakiwafundisha watu uchawi (waliokuwa wakiujua wenyewe tangu zamani), na (uchawi) ulioteremshwa kwa Malaika wawili, Haruta na Maruta, katika (mji wa) Babil. Wala (Malaika hao) hawakumfundisha yo yote mpaka wamwambie: "Hakika sisi ni mtihani (wa kutazamwa kutii kwenu); basi usikufuru." Wakajifunza kwao ambayo kwa mambo hayo waliweza kumfarikisha mtu na mkewe (na mengineyo). Wala hawakuwa wenye kumdhuru yo yote kwa hayo ila kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Na wanajifunza ambayo yatawadhuru wala hayatawafaa. Na kwa yakini wanajua kwamba aliyekhiari haya hatakuwa na sehemu yo yote katika Akhera. Na bila shaka ni kibaya kabisa walichouzia (starehe za) nafsi zao (za Akhera). Laiti wangalijua, (hakika wasingefanya hivi).

وَاتَّبَعُوا مَا تَتْلُو الشَّيَاطِينُ عَلَىٰ مُلْكِ سُلَيْمَانَ ۖ
وَمَا كَفَرَ سُلَيْمَانُ وَلَٰكِنَّ الشَّيَاطِينَ كَفَرُوا يُعَلِّمُونَ
النَّاسَ السِّحْرَ وَمَا أُنزِلَ عَلَى الْمَلَكَيْنِ بِبَابِلَ
هَارُوتَ وَمَارُوتَ ۚ وَمَا يُعَلِّمَانِ مِنْ أَحَدٍ حَتَّىٰ
يَقُولَا إِنَّمَا نَحْنُ فِتْنَةٌ فَلَا تَكْفُرْ ۖ فَيَتَعَلَّمُونَ
مِنْهُمَا مَا يُفَرِّقُونَ بِهِ بَيْنَ الْمَرْءِ وَزَوْجِهِ ۚ وَمَا هُم
بِضَارِّينَ بِهِ مِنْ أَحَدٍ إِلَّا بِإِذْنِ اللَّهِ ۚ وَيَتَعَلَّمُونَ
مَا يَضُرُّهُمْ وَلَا يَنفَعُهُمْ ۚ وَلَقَدْ عَلِمُوا لَمَنِ اشْتَرَاهُ
مَا لَهُ فِي الْآخِرَةِ مِنْ خَلَاقٍ ۚ وَلَبِئْسَ مَا شَرَوْا
بِهِ أَنفُسَهُمْ ۚ لَوْ كَانُوا يَعْلَمُونَ ﴿١٠٢﴾

---

Sahihi za Mtume, kama Ibn Kathir. Tazama Juzuu ya kwanza sahifa 124, hutaiona tafsiri hiyo. Wala Maimamu wa kutaja hadithi sahihi za Mtume-na wakataja tafsiri ya Quran-hawa pia hawakuitaja tafsiri hiyo; ila wametaja kama walivyotaja Maimamu hawa; -Ibn Jarir, Ibn Kathir, Ibnul Mundhir, Al Bayhaqy, Ibn Is-haq na Abu Nunym, kama ilivyo katika sahifa 99 ya Fat-hul Qadyr ya Imam Ash Shaukany. Na ndivyo alivyofasiri Imam Al Bukhary, kama ilivyo katika sahifa 124 ya Juzuu ya 8 ya Fat-hul Bary (Pamoja na kuisoma hiyo Fat-hul Bary). Basi hiyo ya kuwa waliomba kwa jaha ya Mtume siyo NDIYO: ingawa imetajwa na Wafasiri wengi wa nyuma baada ya hao SALAF wa kutegemewa.

Haikuja hadithi ya Mtume SAHIHI inayosema watu wamwombe Mwenyezi Mungu kwa jaha za viumbe Vyake wala majina yao; wala haikusihi katika dua za Mtume dua ya kuomba kwa jaha za viumbe.

Imekuja katika Qurani na Hadithi Sahihi kuombwa Mwenyezi Mungu kwa majina Yake. Basi tufupizike na Alivyotwambia Mwenyezi Mungu na Mtume Wake. Wallahi hatutakuwa watovu kwa kufupizika juu ya haya.

Ama kuomba maiti badala ya kumwomba Mwenyezi Mungu – kama ilivyo katika Dua ya SAALTUKA – haya yamepindukia mipaka-yametia maji maziwani.

93. Muradi ni kuwa walipewa amri lakini hawakuzifuata. Si kuwa walisema kwa mdomo "Tunasikia na tunakataa."

103. Na lau wangeamini na kuogopa, bila shaka malipo yatokayo kwa Mwenyezi Mungu yangekuwa bora kwao. Laiti wangalijua.

وَلَوْ أَنَّهُمْ آمَنُوا وَاتَّقَوْا لَمَثُوبَةٌ مِّنْ عِندِ اللَّهِ
خَيْرٌ ۖ لَّوْ كَانُوا يَعْلَمُونَ ﴿١٠٣﴾

ع ١٢

104. Enyi mlioamini! Msiseme: "Raa'inaa" bali; semeni "Ndhurnaa"; na sikilizeni (amri). Na makafiri watapata adhabu inayoumiza.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَقُولُوا رَاعِنَا وَقُولُوا
انظُرْنَا وَاسْمَعُوا ۗ وَلِلْكَافِرِينَ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿١٠٤﴾

105. Hawapendi waliokufuru miongoni mwa watu waliopewa Kitabu (nao ni Mayahudi na Manasara) wala washirikina, mteremshiwe kheri kutoka kwa Mola wenu. Na Mwenyezi Mungu humteremshia rehema zake amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye fadhila kubwa kabisa.

مَّا يَوَدُّ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ وَلَا
الْمُشْرِكِينَ أَن يُنَزَّلَ عَلَيْكُم مِّنْ خَيْرٍ مِّن رَّبِّكُمْ ۗ
وَاللَّهُ يَخْتَصُّ بِرَحْمَتِهِ مَن يَشَاءُ ۚ
وَاللَّهُ ذُو الْفَضْلِ الْعَظِيمِ ﴿١٠٥﴾

106. Aya yo yote tunayoifuta au kuisahauliza tunaleta iliyo bora kuliko hiyo au iliyo mfano wake. Hujui kwamba Mwenyezi Mungu anao uweza juu ya kila kitu?

مَا نَنسَخْ مِنْ آيَةٍ أَوْ نُنسِهَا نَأْتِ بِخَيْرٍ مِّنْهَا أَوْ مِثْلِهَا ۗ
أَلَمْ تَعْلَمْ أَنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿١٠٦﴾

107. Hujui kwamba Mwenyezi Mungu ni mwenye ufalme wa mbingu na ardhi? Nanyi hamna mlinzi wala hamna msaidizi asiyekuwa Mwenyezi Mungu.

أَلَمْ تَعْلَمْ أَنَّ اللَّهَ لَهُ مُلْكُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ ۗ
وَمَا لَكُم مِّن دُونِ اللَّهِ مِن وَلِيٍّ وَلَا نَصِيرٍ ﴿١٠٧﴾

---

97. Mayahudi, katika hila zao za kumkataa Mtume Muhammad, walimwuliza: "Malaika gani anayekuletea wahyi?" Mtume Akasema: "Jibril". Wakasema: "Lo! Huyo adui yetu, hatumtaki. Lau kuwa Malaika mwingine ndiye anayekuletea Wahyi tungekufuata." Basi Mungu anawajibu hivi.

102. Suleiman aliyetajwa hapa ni Nabii Suleiman. Mayahudi wanamwitakidi Nabii Suleiman kuwa ni mfalme aliyepata ufalme kwa uchawi, si Mtume. Basi na hawa wachawi wa Kiislamu humnasibishia Nabii Suleiman hizo ilimu zao za uchawi. Basi Mwenyezi Mungu anamkanushia haya. Na Aya hii yaonesha wazi kuwa (a) uchawi ni amali ya ukafiri (b) kuwa mchawi hawezi kumdhuru mtu ila kwa idhini ya Mwenyezi Mungu na (c) kuwa mchawi mwenyewe anadhurika kwa uchawi wake.

Na anataja hapa Mwenyezi Mungu kuwa nyuma huko kabisa katika zama za ufalme mkubwa na ustaarabu mkubwa wa Mababiloni (wakazi wa Iraqi wa zamani kabisa), Mwenyezi Mungu aliwaletea Malaika wawili — Harut na Marut — kwa sura ya Kibinaadamu, na wakiwaambia watu kuwa wao wanajua uchawi wa kila namna — wa kuweka na kuondoa, wa kufarikisha na wa kuungamanisha na wa mengine. Lakini wakiwaambia vile vile, "Hapana ruhusa kujifundisha. Atakayekubali tumfundishe atakuwa kafiri; huu ni mtihani mnaofanyiwa na Mwenyezi Mungu; kama mlivyofanyiwa mtihani wa kupewa matamanio ya nafsi na mtihani wa kushindana na Ibilisi na kama hii. Basi huu mtihani. Yazuilieni matamanio yenu, msijifundishe." Lakini wapi! Walijifundisha. Basi huu uchawi ulioko mpaka sasa ni pepesi za uchawi huo. Mwenyezi Mungu anawafanyia viumbe vyake mtihani namna kwa namna ili wadhihiri wema na wajulikane wabaya. Tazama aya ya 155 na 249 katika Suratul Baqarah; na aya ya 166 ya Aali Imran, aya ya 94 ya Al Maida na nyenginezo.

Kwenye maelezo ya Aya waliyoifanya kuwa ni ya 103 wamesema kuwa Nabii Yusuf katika Aya walioifanya ya 32 katika Sura ya 12 (yaani *Surat Yusuf*) alisifiwa na wale wanawake — waliompenda — kwa sifa za Umalaika kwa ajili ya utawa wake. Na anajua huyo mfasiri wa Makadiyani kuwa wamemsifu hivyo kwa ajili ya Uzuri wake uliopindukia mipaka, lakini wamefanya hivi ili wapachikie wanavyotaka kuvipachikia tu kama ilivyo dasturi yao.

104. Waislamu walikuwa wakati mwingine wakimwambia Mtume *"Raainaa"* (Yaani kuwa ukituchunga kama mchungaji mzuri anavyowachunga wanyama wake, kwani sisi ni wajinga, hatujui la madhara wala la maslaha).

108. Je, (nyinyi makafiri wa umma huu); Mnataka kumwuliza Mtume wenu kama alivyoulizwa Musa zamani? Na anayebadilisha Uislamu kwa ukafiri, bila shaka amepotea njia iliyo sawa.

أَمْ تُرِيدُونَ أَنْ تَسْأَلُوا رَسُولَكُمْ كَمَا سُئِلَ مُوسَىٰ
مِنْ قَبْلُ ۗ وَمَنْ يَتَبَدَّلِ الْكُفْرَ بِالْإِيمَانِ فَقَدْ ضَلَّ
سَوَاءَ السَّبِيلِ ﴿١٠٨﴾

109. Wengi miongoni mwa watu waliopewa Kitabu wanapenda wangekurudisheni nyinyi muwe makafiri baada ya kuamini kwenu, kwa sababu ya husuda iliyomo nyoyoni mwao; (iliyowapata) baada ya kuwapambanukia haki. Basi (nyinyi Waislamu) sameheni na puuzeni mpaka Mwenyezi Mungu alete amri yake. Hakika Mwenyezi Mungu ni mwenye uweza juu ya kila kitu.

وَدَّ كَثِيرٌ مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ لَوْ يَرُدُّونَكُمْ مِنْ بَعْدِ إِيمَانِكُمْ
كُفَّارًا حَسَدًا مِنْ عِنْدِ أَنْفُسِهِمْ مِنْ بَعْدِ مَا
تَبَيَّنَ لَهُمُ الْحَقُّ ۖ فَاعْفُوا وَاصْفَحُوا حَتَّىٰ يَأْتِيَ اللَّهُ
بِأَمْرِهِ ۗ إِنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿١٠٩﴾

110. Na simamisheni Sala na toeni Zaka; na kheri mtakazozitanguliza, kwa ajili ya nafsi zenu, mtazikuta kwa Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu anayaona (yote) mnayoyafanya.

وَأَقِيمُوا الصَّلَاةَ وَآتُوا الزَّكَاةَ ۚ وَمَا تُقَدِّمُوا لِأَنْفُسِكُمْ
مِنْ خَيْرٍ تَجِدُوهُ عِنْدَ اللَّهِ ۗ إِنَّ اللَّهَ بِمَا تَعْمَلُونَ
بَصِيرٌ ﴿١١٠﴾

111. Na walisema: "Hataingia Peponi ila aliye Myahudi au Mkristo." Hayo ni matamanio yao tu (si hukumu ya Mungu). Sema: "Leteni dalili zenu, kama nyinyi ni wasema kweli."

وَقَالُوا لَنْ يَدْخُلَ الْجَنَّةَ إِلَّا مَنْ كَانَ هُودًا أَوْ
نَصَارَىٰ ۗ تِلْكَ أَمَانِيُّهُمْ ۗ قُلْ هَاتُوا بُرْهَانَكُمْ إِنْ
كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿١١١﴾

112. Naam, wanaoelekeza nyuso zao kwa Mwenyezi Mungu na wakawa ni watendaji mema (kwa viumbe wenziwao), basi wao watapata malipo yao kwa Mola wao, wala haitakuwa khofu juu yao wala hawatahuzunika.

بَلَىٰ مَنْ أَسْلَمَ وَجْهَهُ لِلَّهِ وَهُوَ مُحْسِنٌ فَلَهُ أَجْرُهُ
عِنْدَ رَبِّهِ وَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿١١٢﴾

113. Na Mayahudi husema: "Wakristo hawana cho chote (cha mategemeo katika dini yao)"; na Wakristo husema: "Mayahudi hawana cho chote (cha mategemeo katika dini yao)"; na hali wote wanasoma Kitabu (walichoteremshiwa bila ya kufuata yaliyomo ndani yake). Na hivi ndivyo wale wasiojua (makafiri wa Kiarabu) wasemavyo. Ni mfano wa kauli yao (wale waliopewa Vitabu. Kila dini moja inatukana dini ya pili). Basi Mwenyezi Mungu atahukumu baina yao siku ya Kiyama katika yale waliyokuwa wakikhitilafiana.

وَقَالَتِ الْيَهُودُ لَيْسَتِ النَّصَارَىٰ عَلَىٰ شَيْءٍ وَقَالَتِ
النَّصَارَىٰ لَيْسَتِ الْيَهُودُ عَلَىٰ شَيْءٍ وَهُمْ يَتْلُونَ
الْكِتَابَ ۗ كَذَٰلِكَ قَالَ الَّذِينَ لَا يَعْلَمُونَ مِثْلَ
قَوْلِهِمْ ۚ فَاللَّهُ يَحْكُمُ بَيْنَهُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ فِيمَا كَانُوا
فِيهِ يَخْتَلِفُونَ ﴿١١٣﴾

114. Na ni nani dhalimu mkubwa kuliko yule anayezuia misikiti ya Mwenyezi Mungu kwamba humo lisitajwe jina lake na akajitahidi kuiharibu?

وَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنْ مَنَعَ مَسَاجِدَ اللَّهِ أَنْ يُذْكَرَ فِيهَا
اسْمُهُ وَسَعَىٰ فِي خَرَابِهَا ۚ

Na tamko hili linashabihi tamko la Kiyahudi ambalo maana yake ni "Wewe mjinga mpotofu!'

Basi Mayahudi wakaona wamepata njia nzuri ya kumtukana Mtume kipunjo pasina mwenyewe kujua wala watu wake kutambua. Ikawa wakifika barazani kwa Mtume hukithirisha kumwambia Mtume *'Raainaa'*; na wanakusudia maana ya 'Wewe mjinga mpotofu!'

Mwenyezi Mungu akakataza kutumiwa hilo tamko la *Raainaa* katika kumsemeza Mtume; Watumie tamko jengine lenye maana ile ile. Nalo *'Ndhurnaa:'* na maana yake ni ile ile ya kuwa 'Tutazame kama mchungaji mwema anavyotazama wanyama wake"

Watu hao haitawafalia kuingia humo misikitini ila kwa kuogopa. (Yaani watieni adhabu kwa ubaya wao huo hata wawe katika khofu). Hao watapata fedheha katika dunia, na katika Akhera watapata adhabu kubwa.

أُولَٰئِكَ مَا كَانَ لَهُمْ أَن يَدْخُلُوهَا إِلَّا خَائِفِينَ ۚ
لَهُمْ فِي الدُّنْيَا خِزْيٌ وَلَهُمْ فِي الْآخِرَةِ عَذَابٌ
عَظِيمٌ ﴿١١٤﴾

115. Na Mashariki na Magharibi ni ya Mwenyezi Mungu. Basi mahala po pote mgeukiapo (alikokuamrisheni Mwenyezi Mungu mtazikuta) huko radhi za Mwenyezi Mungu. Bila shaka Mwenyezi Mungu ni Mwenye wasaa (mkubwa kabisa) na Mwenye kujua (kukubwa kabisa vile vile).

وَلِلَّهِ الْمَشْرِقُ وَالْمَغْرِبُ ۚ فَأَيْنَمَا تُوَلُّوا فَثَمَّ وَجْهُ
اللَّهِ ۚ إِنَّ اللَّهَ وَاسِعٌ عَلِيمٌ ﴿١١٥﴾

---

Wakaikosa Mayahudi fursa hii ya kumtukana Mtume kipunjo mbele ya macho yake na mbele ya watu wake.

106. Baadhi ya Mifano ya hukumu zilizonasikhiwa (zilizofutwa) kwa hukumu nyingine ni ulevi. (a) Ulevi ulikuwa halali kabla ya kuja Uislamu. Kisha ukaharimishwa nyakati za Sala. Kisha ukaharimishwa kabisa. (b) Sala ilikuwa Asubuhi na Jioni tu. Kisha ikawa mara tano. (c) Katika kufunga ilikuwa pana khiari. Mtu akitaka atafunga na akitaka atatoa sadaka ya chakula awape masikini badala ya kufunga. Kisha ikawa lazima kufunga maadam hana udhuru wo wote.

Kwenye maelezo ya Aya walioihisabu kuwa ni ya 107 (na khasa ilivyo ni Aya 106) wamekanusha habari ya Naskh, wakasema kuwa Aya za Quran hazipingani. Hapana shaka kuwa Aya za Quran hazipingani. Lakini amri zake — na khasa makatazo yake — hazikuwa zikiamrisha jambo na kulikataza kwa ghafla. Lakini mara nyingi huliamrisha kidogo kidogo na kulikataza kwa daraja — kidogo kidogo. Na hivi ndivyo kila mwenye hikima anavyofanya. Na Mwenyezi Mungu kajisifu mara nyingi katika Quran kuwa ni Mwenye hikima na Mambo Yake Yote anayafanya kwa Hikima. Na Kuamrisha kidogo kidogo na kukataza kidogo kidogo ndiyo Hikima. Na mifano tulioitoa katika maelezo ya Aya hii inatosha kuonyesha uwongo wa kukataa kwao Naskh. Na Aya hii ya 106 inaonyesha dhahiri haya wanayoyasema ulamaa wanaokubalisha Naskh.

108. Watu wa Nabii Musa walimfanyia vihendo vingi Nabii Musa—vya kumtaka hiki na hiki; hata walimtaka (a) Amtake Mwenyezi Mungu Awasemeze na (b) Waonane naye. Basi na hawa makafiri wa Kiqureshi walianza nao kutaka kama hawa.

114. Mtume alipokuwa Makka Maqureshi wakimzuilia asisali katika Al-Kaaba yeye wala watu wake. Na baada ya kuwa wako Madina walifunga safari kuja Makka kufanya ibada, Maqureshi wakawazuilia vile vile.

Maelezo yaliyo sahihi ya Aya walioifanya kuwa ni ya 115 (na hakika ni ya 114) ni yale waliyoyatia mwanzo kabisa katika maelezo ya Aya walioifanya kuwa ni ya 116. Maelezo waliyoyatia katika hiyo waliyoifanya kuwa ni ya 115 ni ya Propaganda tu ya dini yao — isiyokubaliwa na Uislamu. Dini yao wenyewe waliyoizua. Uislamu haumkubalishii mtu kupewa Utume BAADA ya Nabii Muhammad. Na tumekwisha kutaja habari hii katika kurejeza maelezo ya Aya ya 4 ya sura hii hii.

115. Wamepachika ya uwongo tena katika maelezo ya Aya waliyoifanya kuwa ni ya 116, nayo ni ya 115. Kwanza wamesema kuwa huyo Mirza Ghulam wao, aliyezaliwa Bara Hindi kwenye kitaa cha Kadiyan (Punjab); aliyezaliwa na baba na mama wa Kihindi; akawako ulimwenguni kisha akafa kiasi cha miaka mia sasa. Wamesema kuwa huyo ndiye huyo Masihubni Maryam (Nabii Isa) aliyetajwa katika Quran na Hadithi za Mtume aliyezaliwa Falastin (Palestine) na mama wa Kiisrail pasina baba, (kazaliwa kwa Muujiza) ambaye aliishi ulimwenguni siku za kuishi kisha akaondoka kiasi cha miaka alfu mbili sasa; na akasema Mtume kuwa mwisho wa ulimwengu atarejea kwa muujiza vile vile kama alivyozaliwa kwa muujiza na akaondoka kwa muujiza. Makadiyani wanasema katika hii tafsiri yao kuwa Masihi aliyetajwa na Mwenyezi Mungu na Mtume ndiye Mirza Ghulam wao! Maneno haya ni ya kichaa na wazimu. Na ni wazimu mtu kujibizana na wanaojitia — kusudi — kichaa na wazimu, ili wawatie watu wazimu. Wazimu utaambaa kichaka cha Uislamu, uwasawawe wao wenyewe tu. Wanajitia wazimu makusudi na pambani ili wawapambanize watu na dini yao ya haki! Watapambanika wabaranganyike wao wenyewe.

Pa pili walipopoongezea ni kusema kwao: "Mtume s.a.w. alisema ya kwamba katika wakati wa Masih-ul-Mawuud jua litakucha toka Magharibi". Uwongo kabisa. Hakuna kabisa katika Hadithi za Mtume tamko la Masih ul-Mawuud. Hii ni tamko wanalompachikia nalo huyo Ghulam wao. Tamko la Masih ul-Mawuud halimo katika Quran wala Hadithi za Mtume. Humo mna tamko la Masihu tupu. Au Masihubn Maryam. Na katika Hadithi za Mtume liko vile vile tamko la Masihud Dajjal — Potezaji kubwa litakalokuja mwisho wa ulimwengu.

116. Na (makafiri) wanasema: "Mwenyezi Mungu amejifanyia mtoto." Ameepukana na hilo (Mwenyezi Mungu); bali ni (viumbe) vyake (tu vyote) hivyo vilivyomo mbinguni na ardhini (si watote wake). Vyote vinamtii yeye (kwa utumwa).

وَقَالُوا اتَّخَذَ اللّٰهُ وَلَدًا ۙ سُبْحٰنَهٗ ؕ بَلْ لَّهٗ مَا
فِی السَّمٰوٰتِ وَ الْاَرْضِ ؕ كُلٌّ لَّهٗ قٰنِتُوْنَ ﴿۱۱۶﴾

117. (Yeye ndiye) Muumba wa mbingu na ardhi pasina ruwaza; na anapotaka jambo basi huliambia tu, "Kuwa"; nalo huwa.

بَدِیْعُ السَّمٰوٰتِ وَ الْاَرْضِ ؕ وَ اِذَا قَضٰۤی اَمْرًا
فَاِنَّمَا یَقُوْلُ لَهٗ كُنْ فَیَكُوْنُ ﴿۱۱۷﴾

118. Na walisema wale wasiojua (kitu), (yaani Makafiri wa Kiqureshi): "Mbona Mwenyezi Mungu hasemi nasi au kutufikia hoja (tunazozitaka)?" Vivyo hivyo walisema wale waliokuwa kabla yao, mfano wa kauli yao hii; nyoyo zao zimefanana. Hakika Sisi tumezibainisha hoja (zetu zote; zimewabainikia) kwa watu wenye kuyakinisha mambo.

وَقَالَ الَّذِیْنَ لَا یَعْلَمُوْنَ لَوْلَا یُكَلِّمُنَا اللّٰهُ
اَوْ تَاْتِیْنَاۤ اٰیَةٌ ؕ كَذٰلِكَ قَالَ الَّذِیْنَ مِنْ قَبْلِهِمْ
مِّثْلَ قَوْلِهِمْ ؕ تَشَابَهَتْ قُلُوْبُهُمْ ؕ قَدْ بَیَّنَّا الْاٰیٰتِ
لِقَوْمٍ یُّوْقِنُوْنَ ﴿۱۱۸﴾

119. Hakika sisi tumekutuma ubainishe haki, kwa kubashiri na kuonya, wala hutaulizwa watu wa Motoni (kwa nini wakaingia Motoni).

اِنَّاۤ اَرْسَلْنٰكَ بِالْحَقِّ بَشِیْرًا وَّ نَذِیْرًا ۙ وَّ لَا تُسْـَٔلُ
عَنْ اَصْحٰبِ الْجَحِیْمِ ﴿۱۱۹﴾

120. Hawatakuwa radhi juu yako Mayahudi wala Wakristo mpaka ufuate mila yao. Sema: "Hakika uwongozi wa Mwenyezi Mungu ndio uwongozi (khasa)." Na kama ukifuata matamanio yao baada ya yale yaliyokufikia ya ujuzi (wa kweli) hutapata msaidizi yo yote wala mlinzi kwa Mwenyezi Mungu.

وَلَنْ تَرْضٰی عَنْكَ الْیَهُوْدُ وَ لَا النَّصٰرٰی حَتّٰی
تَتَّبِعَ مِلَّتَهُمْ ؕ قُلْ اِنَّ هُدَی اللّٰهِ هُوَ الْهُدٰی ؕ
وَ لَئِنِ اتَّبَعْتَ اَهْوَآءَهُمْ بَعْدَ الَّذِیْ جَآءَكَ مِنَ
الْعِلْمِ ۙ مَا لَكَ مِنَ اللّٰهِ مِنْ وَّلِیٍّ وَّ لَا نَصِیْرٍ ﴿۱۲۰﴾

121. Wale (katika Ahlil Kitabu) tuliowapa Kitabu (Taurati, Injili, Zaburi, . . .) wakakisoma

اَلَّذِیْنَ اٰتَیْنٰهُمُ الْكِتٰبَ یَتْلُوْنَهٗ حَقَّ تِلَاوَتِهٖ ؕ

---

Labda chanzo chake ni huyu mtu wao — Mirza Ghulam — wanayemwita Masih ul-Mawuud. Basi uwongo mpachiko wao huu. Hakutamka Mtume tamko hilo la Masihul Mawuud. Nawatuonyeshe Hadithi hiyo katika vitabu vya Hadithi vya kutegemewa.

Mtume alisema kuwa moja katika alama za kufika Kiyama ni kutoka jua Magharibi likachwa Mashariki, kama alivyosema — na Mwenyezi Mungu pia — kuwa nyota zitapukutika, bahari zitachanganyika, bahari zitawaka moto, wanyama wote watakusanyika pamoja kwa khofu. Na kama haya. Na yakisha kufika haya hapatachukua muda. Mara ulimwengu utakwisha. Wao wanasema kuwa Jua ndilo limekwisha kuchomoza Magharibi kwa kuja Mkadiyani wao huyo! Mbona basi ulimwengu haujesha? Na tangu kuja Mkadiyani wao huyo ni kiasi cha miaka mia sasa. Uwongo! Wana nyuso kavu kweli kweli, zisizokuwa na Zaibaki hata chembe! Hawana haya kusema uwongo ulio dhahir shahir. Na kuzua uwongo wa dhahir shahir kama hivi ni alama ya kutoamini maneno ya Mungu kama alivyosema Mwenyewe Mwenyezi Mungu katika Aya ya 105 ya *Suratun Nahl*. Natutahadhari na uwongo wao hawa ambao hamu yao ni kuwapoteza Waislamu. Wametoka kwao huko Bara Hindi kuja huku — na kwingineko — wawapoteze Waislamu tu. Na huko kujiita kwao *waislamu* ni kujirembaremba tu ili wadhihiri kuwa Waislamu; kama wanavyojiremba wacheza Kiluwa na Kumba na Kisonge na zilizo kama hizi. Na hao wacheza ngoma hizo wanafanya hayo kwa mchezo tu, sio kuwakhadaa watu. Lakini Makadiyani wanajiremba hivyo kwa ajili ya kuwapoteza watu na dini yao ya haki.

Pa tatu pa uwongo walipopapachika—hali ya kuwa macho ya walimwengu wote yanawasuta na kope zinawasusuwika—ni kusema kwao: "Na sasa katika zama za Masihi wake, Seyyidna Ahmad (walitia dua) utaenea (yaani Uislamu) pande za magharibi yaani Ulaya na America."

Waongo wakubwa Makadiyani wapotezaji watu wajinga. Ati Uislamu umebashiriwa na Mwenyezi Mungu na Mtumewe kuwa utaingia kidogo kidogo katika Ulaya na America katika zama za Ghulam wao, na hali ya kuwa

أُولَٰئِكَ يُؤْمِنُونَ بِهِ ۗ وَمَن يَكْفُرْ بِهِ
فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْخَاسِرُونَ ﴿١٢١﴾

kama ipasavyo kukisoma (bila ya kupotoa tafsiri yake wala kutoa hili na kutia lile), hao huiamini hii (Quran wakasilimu). Na wanaokikanusha (hicho Kitabu chao wakapinduapindua tafsiri yake na wakaongeza na wakapunguza), basi hao ndio wenye hasara.

يَا بَنِي إِسْرَائِيلَ اذْكُرُوا نِعْمَتِيَ الَّتِي أَنْعَمْتُ
عَلَيْكُمْ وَأَنِّي فَضَّلْتُكُمْ عَلَى الْعَالَمِينَ ﴿١٢٢﴾

122. Enyi kizazi cha Israili (Mayahudi)! Kumbukeni neema Zangu nilizokuneemesheni, na (kumbukeni) nilivyokufadhilisheni juu ya viumbe wengine (wote waliokuwa zama hizo).

وَاتَّقُوا يَوْمًا لَّا تَجْزِي نَفْسٌ عَن نَّفْسٍ شَيْئًا وَلَا
يُقْبَلُ مِنْهَا عَدْلٌ وَلَا تَنفَعُهَا شَفَاعَةٌ وَلَا هُمْ
يُنصَرُونَ ﴿١٢٣﴾

123. Na iogopeni siku ambayo nafsi haitaifaa kitu nafsi nyingine, wala hakitakubaliwa kikomboleo kwake; wala maombezi hayataifaa, wala hawatanusuriwa.

وَإِذِ ابْتَلَىٰ إِبْرَاهِيمَ رَبُّهُ بِكَلِمَاتٍ فَأَتَمَّهُنَّ ۖ قَالَ إِنِّي
جَاعِلُكَ لِلنَّاسِ إِمَامًا ۖ قَالَ وَمِن ذُرِّيَّتِي ۖ
قَالَ لَا يَنَالُ عَهْدِي الظَّالِمِينَ ﴿١٢٤﴾

124. Na (kumbukeni khabari hii:) Mola wake alipomfanyia mtihani (Nabii) Ibrahim kwa amri nyingi; naye akazitimiza. Akamwambia: "Hakika mimi nitakufanya kiongozi wa watu (wote)." (Ibrahim akasema:) "Je, na katika kizazi changu pia?" Akasema: "(Ndio lakini) ahadi Yangu haitawafikia (waovu) madhalimu wa nafsi zao"; (itawafikia walio wazuri).

وَإِذْ جَعَلْنَا الْبَيْتَ مَثَابَةً لِّلنَّاسِ وَأَمْنًا ۗ
وَاتَّخِذُوا مِن مَّقَامِ إِبْرَاهِيمَ مُصَلًّى ۖ وَعَهِدْنَا
إِلَىٰ إِبْرَاهِيمَ وَإِسْمَاعِيلَ أَن طَهِّرَا بَيْتِيَ
لِلطَّائِفِينَ وَالْعَاكِفِينَ وَالرُّكَّعِ السُّجُودِ ﴿١٢٥﴾

125. Na (kumbukeni khabari hii pia:) Tulipoifanya nyumba (ya Al-Kaaba) iwe mahali pa kuendewa na watu na mahali pa salama. Na mahali alipokuwa akisimama Ibrahimu pafanyeni pawe pa kusalia. Na tulimwusia Ibrahimu na Ismaili (tukawaambia): "Itakaseni (isafisheni) nyumba yangu kwa ajili ya wale wanaoizunguka kwa ajili ya kutufu na wanaokaa hapo na (kwa ajili ya) wanaorukuu na kusujudu hapo pia."

---

Ghulam wao huyu kazaliwa katika hii karne ya Kumi na Nane ya Masihi, 1800 A.D. Makadiyani waliosoma wanajua—na kila mwenye kusoma tarekhe ya Uislamu anajua — kuwa Uislamu umeingia katika Ulaya (Spain, Portugal, France, Italy) tangu zama za Matabiina katika dola ya Bani Umayya katika karne ya Mia Saba ya Masihi, 700 A.D. Na umeingia Ulaya Greece, Albania, Rumania, Bulgaria, Hungary, Poland, Yugoslavia na kwengineko tangu katika nguvu za dola ya Kiturky katika karne ya Kumi na Nne ya Kimasihi, 1400 A.D. Na mpaka leo sehemu nyingi za nchi hizi zina Uislamu wao. Nende yoyote huko atayaona haya. Wao wanajidai kuwa Uislamu umeanza kuingia Ulaya zama za Mkadiyani wao. Wao wanadhani kuwa kila mtu katika nchi hizi ni mjinga; wa kumchezea. Wamehizika. Hawawezi kutula Bunga, isipokuwa wachache wanaowaghuri kwa ambayo hatupendi kuyasema. Lakini kila mtu anajua. Na mwenye macho haambiwi tazama. Tazama uwongo wao huu! Hawana haya hata chembe kwenda kuupachika humu katika hii wanayoita Maelezo; kumbe Mapotezo. Wataendelea wenyewe tu kujipoteza; hawatampoteza mwingine inshallah. Na America umefika Uislamu kabla ya Columbus kufika huko kwenye mwisho wa karne ya 1400 A.D.

116. Wakristo wanadai kuwa wanamwita Isa mtoto wa Mungu kwa sababu ati Mwenyezi Mungu Amemwita "Mwanawe" (kama ilivyo katika vitabu vyao). Lakini ukisoma vitabu vyao utaona kuwa Adam pia ameitwa mwana wa Mungu, na wala Wakristo hawaamini kuwa ni mwanawe. Tazama Luka 3:38. Hapana shaka kuwa "uwana" huu ni wa huruma na mapenzi tu, kama vile mtu amwitavyo "mwanangu" mtumishi wake ampendaye. Si "uwana" wa kizazi.

118. Maqureshi walimwambia Mtume Muhammad kuwa hawatamkubali kuwa Mtume mpaka Mwenyezi

126. Na (kumbukeni khabari hii nayo:) aliposema Ibrahimu: "Ee Mola wangu! Ufanye mji huu (wa Makka) uwe wa salama na uwape wakazi wake matunda; wale wanaomwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho." (Mwenyezi Mungu) akasema: "Na mwenye kukufuru (pia) nitamstarehesha kidogo, kisha nitamsukumiza katika adhabu ya Moto, napo ni mahali pabaya kabisa pa kurejea."

وَإِذْ قَالَ إِبْرٰهِمُ رَبِّ اجْعَلْ هٰذَا بَلَدًا اٰمِنًا
وَّارْزُقْ أَهْلَهُ مِنَ الثَّمَرٰتِ مَنْ اٰمَنَ مِنْهُمْ بِاللّٰهِ
وَالْيَوْمِ الْاٰخِرِ ۚ قَالَ وَمَنْ كَفَرَ فَأُمَتِّعُهُ قَلِيلًا
ثُمَّ أَضْطَرُّهُ إِلٰى عَذَابِ النَّارِ ۚ وَبِئْسَ الْمَصِيرُ ﴿١٢٦﴾

127. Na (kumbukeni khabari hii pia:) Ibrahimu alipoinua kuta za nyumba (hii ya Al-Kaaba) na Ismaili (pia); (wakaomba wakasema:) "Ee Mola wetu! Tutakabalie (amali yetu hii ya kujenga huu msikiti). Hakika wewe ndiye Mwenye kusikia, na Mwenye kujua."

وَإِذْ يَرْفَعُ إِبْرٰهِمُ الْقَوَاعِدَ مِنَ الْبَيْتِ
وَإِسْمٰعِيلُ ۚ رَبَّنَا تَقَبَّلْ مِنَّا ۚ إِنَّكَ أَنْتَ
السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿١٢٧﴾

128. "Ee, Mola Wetu! Utufanye tuwe wanyenyekevu kwako. Na miongoni mwa kizazi chetu (pia ufanye) umma mnyenyekevu kwako. Na utuonyeshe njia ya ibada yetu na utusamehe. Bila shaka Wewe ndiye Mwenye kusamehe na Mwenye kurehemu."

رَبَّنَا وَاجْعَلْنَا مُسْلِمَيْنِ لَكَ وَمِنْ ذُرِّيَّتِنَا
أُمَّةً مُّسْلِمَةً لَّكَ ۖ وَأَرِنَا مَنَاسِكَنَا وَتُبْ
عَلَيْنَا ۚ إِنَّكَ أَنْتَ التَّوَّابُ الرَّحِيمُ ﴿١٢٨﴾

129. "Ee, Mola wetu! Waletee Mtume anayetokana na wao, awasomee Aya Zako, na kuwafundisha Kitabu (chako) na hikima (nyingine) na awafundishe kujitakasa (na kila mabaya). Hakika Wewe ndiye Mwenye nguvu, na ndiye Mwenye hikima.

رَبَّنَا وَابْعَثْ فِيهِمْ رَسُولًا مِّنْهُمْ يَتْلُوا عَلَيْهِمْ اٰيٰتِكَ
وَيُعَلِّمُهُمُ الْكِتٰبَ وَالْحِكْمَةَ وَيُزَكِّيهِمْ ۚ إِنَّكَ أَنْتَ
الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿١٢٩﴾ ع ١٥

130. Na nani atajitenga na mila ya Ibrahimu (akaichukia dini hii ya Kiislamu) isipokuwa anayeitia nafsi yake katika upumbavu? Na kwa yakini sisi tulimchagua (Ibrahimu) katika dunia; na kwa hakika yeye katika Akhera atakuwa miongoni mwa watu wema (kabisa).

وَمَنْ يَّرْغَبُ عَنْ مِّلَّةِ إِبْرٰهِمَ إِلَّا مَنْ سَفِهَ
نَفْسَهُ ۚ وَلَقَدِ اصْطَفَيْنٰهُ فِي الدُّنْيَا ۖ وَإِنَّهُ فِي
الْاٰخِرَةِ لَمِنَ الصّٰلِحِينَ ﴿١٣٠﴾

131. (Kumbukeni habari hii:) Mola wake alipomwambia: "Nyenyekea;" akanena "Nimenyenyekea kwa Mola wa walimwengu (wote)".

إِذْ قَالَ لَهُ رَبُّهُ أَسْلِمْ ۙ قَالَ أَسْلَمْتُ
لِرَبِّ الْعٰلَمِينَ ﴿١٣١﴾

132. Na Ibrahimu akawausia haya wanawe; na Yaakubu (pia akawausia wanawe): "Enyi wanangu! Hakika Mwenyezi Mungu amekuchagulieni dini hii; basi msife ila nanyi mmekuwa wanyenyekevu."

وَوَصّٰى بِهَا إِبْرٰهِمُ بَنِيهِ وَيَعْقُوبُ ۚ يٰبَنِيَّ
إِنَّ اللّٰهَ اصْطَفٰى لَكُمُ الدِّينَ فَلَا تَمُوتُنَّ إِلَّا
وَأَنْتُمْ مُّسْلِمُونَ ﴿١٣٢﴾ ط

133. Je; (nyinyi Mayahudi na Manasara) mlikuwapo yalipomfikia Yaakubu mauti, alipowaambia wanawe: "Je, mtamuabudu nani

أَمْ كُنْتُمْ شُهَدَاءَ إِذْ حَضَرَ يَعْقُوبَ الْمَوْتُ ۙ
إِذْ قَالَ لِبَنِيهِ مَا تَعْبُدُونَ مِنْ بَعْدِي ۖ قَالُوا نَعْبُدُ

Mungu awakabili uso kwa uso, *Subhanahuuwa Ta'ala*, awaambie kuwa 'Kweli Muhammad ni mjumbe Wangu.' Na walitaka vihendo (vitimvi) vingi vinginevyo kama hivi.

124. Nabii Ibrahim alipofanyiwa mitihani yote ya amri za Mwenyezi Mungu na makatazo yake na ya mambo

إِلَٰهَكَ وَإِلَٰهَ آبَائِكَ إِبْرَاهِيمَ وَإِسْمَاعِيلَ وَإِسْحَاقَ
إِلَٰهًا وَاحِدًا وَنَحْنُ لَهُ مُسْلِمُونَ ﴿١٣٣﴾

baada yangu?" Wakasema: "Tutamwabudu Mola wako na Mola wa baba zako, Ibrahimu na Ismaili na Is-haka; Mungu Mmoja tu, na sisi tunanyenyekea kwake."

تِلْكَ أُمَّةٌ قَدْ خَلَتْ لَهَا مَا كَسَبَتْ وَلَكُم مَّا
كَسَبْتُمْ وَلَا تُسْأَلُونَ عَمَّا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٣٤﴾

134. Hao ni watu waliokwishapita, (hapana faida kujitapa nao). Watapata waliyoyachuma, nanyi mtapata mtakayoyachuma, wala hamtaulizwa nyinyi waliyokuwa wakiyafanya wao. (Kila mmoja ataulizwa alipwe kwa alilolifanya mwenyewe).

وَقَالُوا كُونُوا هُودًا أَوْ نَصَارَىٰ تَهْتَدُوا قُلْ بَلْ مِلَّةَ
إِبْرَاهِيمَ حَنِيفًا وَمَا كَانَ مِنَ الْمُشْرِكِينَ ﴿١٣٥﴾

135. Na wakasema: (Mayahudi kuwaambia Waislamu): "Kuweni Mayahudi (mtaongoka)" (na wakasema Manasara nao kuwaambia Waislamu) au (Kuweni) Wakristo mtaongoka." Sema: "Bali (tunashika) mila ya Ibrahimu aliyewacha dini za upotofu akashika dini ya haki, wala hakuwa (kabisa) katika washirikina."

قُولُوا آمَنَّا بِاللَّهِ وَمَا أُنزِلَ إِلَيْنَا وَمَا أُنزِلَ إِلَىٰ
إِبْرَاهِيمَ وَإِسْمَاعِيلَ وَإِسْحَاقَ وَيَعْقُوبَ وَالْأَسْبَاطِ
وَمَا أُوتِيَ مُوسَىٰ وَعِيسَىٰ وَمَا أُوتِيَ النَّبِيُّونَ
مِن رَّبِّهِمْ لَا نُفَرِّقُ بَيْنَ أَحَدٍ مِّنْهُمْ وَنَحْنُ
لَهُ مُسْلِمُونَ ﴿١٣٦﴾

136. Semeni nyinyi (Waislamu waambiwe Mayahudi na Manasara; waambieni): "Tumemwamini Mwenyezi Mungu na yale tuliyoteremshiwa, na yale yaliyoteremshwa kwa Ibrahimu na Ismaili na Is-haqa na Yaaqubu na kizazi (chake Yaaqubu); na waliyopewa Musa na Isa na pia yale waliyopewa Manabii (wengine) kutcka kwa Mola wao; hatutafautishi baina ya yo yote katika hao. (Wote tunawaamini); na sisi tumenyenyekea kwake."

فَإِنْ آمَنُوا بِمِثْلِ مَا آمَنتُم بِهِ فَقَدِ اهْتَدَوا
وَّإِن تَوَلَّوْا فَإِنَّمَا هُمْ فِي شِقَاقٍ
فَسَيَكْفِيكَهُمُ اللَّهُ وَهُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿١٣٧﴾

137. Basi wakiamini hao (Manasara na Mayahudi) kama mnavyoamini (nyinyi), itakuwa kweli wameongoka. Na wakikengeuka basi wao wamo katika upinzani tu. Basi Mwenyezi Mungu atakukinga na shari yao, na Yeye ndiye asikiaye na ajuaye.

صِبْغَةَ اللَّهِ وَمَنْ أَحْسَنُ مِنَ اللَّهِ صِبْغَةً
وَنَحْنُ لَهُ عَابِدُونَ ﴿١٣٨﴾

138. (Uislamu ni) pambo la Mwenyezi Mungu (alilotupamba. Kuweni na nyinyi Waislamu;). Na ni nani aliye mzuri kwa kupamba kuliko Mwenyezi Mungu? Na sisi tunamuabudu yeye tu.

قُلْ أَتُحَاجُّونَنَا فِي اللَّهِ وَهُوَ رَبُّنَا وَرَبُّكُمْ

139. Sema (Ee Muhammad uwaambie Mayahudi na Manasara): "Oh! Mnahojiana nasi juu ya jambo

---

mengine, na akafuzu; Mwenyezi Mungu alimwambia kuwa kampa daraja ya Uimamu juu ya viumbe. Nabii Ibrahim alifurahi akashukuru na akamwomba kuwa na katika kizazi chake wapewe Uimamu pia. Mwenyezi Mungu akamwambia kuwa Nasaba tupu ya kunasibika naye (Nabii Ibrahimu) haitakuwa sababu ya kuwapatia Uimamu—sharti wafanye amali nzuri.

Na yote haya ni kufundishwa na sisi pia kuwa tusitegemee nasabu zetu. Siyo nguzo ya kwegema (kuegemea) 'Nguzo ya kwegema ni amali njema zinazofanywa kwa nia njema.' Mtume kasema: "Mwenyezi Mungu hatazami sura zenu wala mali yenu lakini anatazama nyoyo zenu na amali zenu." Tazama aya ya 80 ya sura hii hii.

Wamedokeza tena upotezi wao katika maelezo ya Aya waliyoihisabu kuwa ni ya 125 (Nayo ni ya 124). Waliandika hivi: "Nabii Ibrahimu alipopewa unabii, aliomba wazao wake nao wapewe neema hiyo. Mwenyezi Mungu alikubali kuwa, ndiyo, unabii utaendelea. . ." Wamepachika haya makusudi ili kumthibitishia huyo Ghulam wao Utume wanaomdaia! Lakini haya kaambiwa Nabii Ibrahimu — kiasi cha miaka elfu tano sasa

وَلَنَآ أَعْمَٰلُنَا وَلَكُمْ أَعْمَٰلُكُمْ
وَنَحْنُ لَهُۥ مُخْلِصُونَ ﴿١٣٩﴾

la Mwenyezi Mungu" (kwa nini Utume ukaja upande wetu)? Na hali Yeye ni Mola wetu na Mola wenu? (Mlipokuwa wazuri alikupeni nyinyi. Na mlipoharibika katupa sisi). Na sisi tuna vitendo vyetu, nanyi mna vitendo vyenu; nasi tunajihalisisha kwake tu. (Nyinyi mnaabudu Masanamu)

أَمْ تَقُولُونَ إِنَّ إِبْرَٰهِـۧمَ وَإِسْمَٰعِيلَ وَإِسْحَٰقَ
وَيَعْقُوبَ وَٱلْأَسْبَاطَ كَانُوا۟ هُودًا أَوْ نَصَٰرَىٰ ۗ
قُلْ ءَأَنتُمْ أَعْلَمُ أَمِ ٱللَّهُ ۗ وَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّن كَتَمَ
شَهَٰدَةً عِندَهُۥ مِنَ ٱللَّهِ ۗ وَمَا ٱللَّهُ بِغَٰفِلٍ عَمَّا
تَعْمَلُونَ ﴿١٤٠﴾

140. Mnasema (nyinyi Mayahudi na Manasara) kuwa Ibrahimu na Ismaili na Is–haqa na Yaaqubu na kizazi (chake) walikuwa Mayahudi (kama nyinyi) au Wakristo (kama nyinyi)? Sema: "Je, nyinyi mnajua zaidi au Mwenyezi Mungu? Na ni nani dhalimu mkubwa kuliko yule afichae ushahidi alio nao utokao kwa Mwenyezi Mungu? Na Mwenyezi Mungu si Mwenye kughafilika na hayo mnayoyafanya."

تِلْكَ أُمَّةٌ قَدْ خَلَتْ ۖ لَهَا مَا كَسَبَتْ وَلَكُم مَّا
كَسَبْتُمْ ۖ وَلَا تُسْـَٔلُونَ عَمَّا كَانُوا۟ يَعْمَلُونَ ﴿١٤١﴾

141. Hao ni watu waliokwishapita. (Hapana faida kujitapa kwa ajili yao). Wao watapata waliyoyachuma, na nyinyi mtapata mliyoyachuma, wala hamtaulizwa nyinyi yale waliyokuwa wakifanya wao; (wala wao hawataulizwa walipwe kwa mnayoyafanya nyiye. Kila mtu atalipwa kwa lake).

سَيَقُولُ ٱلسُّفَهَآءُ مِنَ ٱلنَّاسِ مَا وَلَّىٰهُمْ عَن
قِبْلَتِهِمُ ٱلَّتِى كَانُوا۟ عَلَيْهَا ۚ قُل لِّلَّهِ ٱلْمَشْرِقُ وَ
ٱلْمَغْرِبُ ۚ يَهْدِى مَن يَشَآءُ إِلَىٰ صِرَٰطٍ مُّسْتَقِيمٍ ﴿١٤٢﴾

142. Karibuni wapumbavu miongoni mwa watu watasema: "Nini kilichowageuza kutoka kibla chao walichokuwa wakikielekea?" Sema: (uwaambie) "Mashariki na Magharibi ni ya Mwenyezi Mungu; humwongoza amtakae katika njia iliyonyoka."

وَكَذَٰلِكَ جَعَلْنَٰكُمْ أُمَّةً وَسَطًا لِّتَكُونُوا۟ شُهَدَآءَ
عَلَى ٱلنَّاسِ وَيَكُونَ ٱلرَّسُولُ عَلَيْكُمْ شَهِيدًا ۗ وَمَا

143. Na vivyo hivyo tumekufanyeni umati bora (kama kibla chenu tulivyokifanya bora) ili muwe mashahidi juu ya watu, na Mtume awe shahidi juu yenu. Na hatukukifanya kibla ulichokuwa nacho

---

(5000). Wamekuja baada yake chungu ya Mitume, hata anaitwa Baba wa Mitume. Khalafu baada ya Kupita miaka yote hiyo ndio imeambiwa katika Quran na Hadithi za Mtume—kama tulivyobainisha katika maelezo ya Aya ya 4 ya *Suratul Baqarah*—kuwa sasa baada ya Nabii Muhammad hapewi tena mtu mwengine Utume. Watafedheheka tu maisha Makadiyani na watahizika, kwani wanaitafuta wenyewe hizaya. Na haambiwi "Pole" mtu kwa ugonjwa wa kujitakia.

126. Nabii Ibrahimu alipoiombea kheri nchi ya Makka na akawaombea riziki wakazi wake, aliwaombea wale Waislamu tu. Mwenyezi Mungu akamwambia "La, ukubwa wa dini mbali na riziki mbali. Ukubwa wa dini ndio haupati ila mwema. Ama riziki hapa duniani nitampa yo yote yule, akiwa Mwislamu au akiwa si Mwislamu."

133. Mayahudi walimkanusha Mtume alipowaambia kuwa Nabii Yaaqubu aliwausia watoto wake kufuata Uislamu. Basi Mwenyezi Mungu ndiyo anawaambia "Mlikuwapo nyinyi hata mnakanusha?"

136. Aya hii mara nyingi Mtume akiisoma katika rakaa ya mwanzo ya suna ya Al-fajiri(kabliya), na akisoma katika rakaa ya pili aya ya 64 ya Surat aali-Imran.

138. Watoto wa Kikristo hubatizwa (huchovywa ndani ya maji wanayoyaitakidi kuwa matakatifu). Basi hapo huitakidiwa kuwa washapakika Ukristo. Ndio wanaambiwa hapa kuwa dini ya Kiislamu ni dini inayowafiki tabia (Nature) ya binaadamu wote. Basi nawapakike hii rangi aliyowapaka Mwenyewe Mwenyezi Mungu.

139. Mayahudi na Manasara waliwaambia Waislamu kuwa "Uwongo, Muhammad si Mtume, kwani Mitume hutokana na Mayahudi." Basi ndiyo wakaambiwa wawambie kuwa "Kwani Mola si huyo mmoja tu, na sisi sote si watumwa wake? Si yo yote yule atakayekwenda mwendo mzuri atapendwa na apewe fadhila na Mola wake? Sharti awe Yahudi?"

(mara ya kwanza kuwa ndiyo kibla chako sasa na mpaka mwisho wa ulimwengu) ila tupate kumjulisha (atambulikane) yule anayemfuata Mtume na yule anayegeuka akarejea nyuma. Na kwa yakini lilikuwa jambo gumu isipokuwa kwa wale aliowaongoza Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu hakuwa mwenye kuipoteza imani yenu. Kwani Mwenyezi Mungu kwa watu ni Mpole sana (na) mwenye rehema.

جَعَلْنَا الْقِبْلَةَ الَّتِي كُنْتَ عَلَيْهَا إِلَّا لِنَعْلَمَ مَنْ
يَتَّبِعُ الرَّسُولَ مِمَّنْ يَنْقَلِبُ عَلَىٰ عَقِبَيْهِ ۚ وَإِنْ
كَانَتْ لَكَبِيرَةً إِلَّا عَلَى الَّذِينَ هَدَى اللَّهُ ۗ وَمَا كَانَ
اللَّهُ لِيُضِيعَ إِيمَانَكُمْ ۚ إِنَّ اللَّهَ بِالنَّاسِ لَرَءُوفٌ رَحِيمٌ ﴿١٤٣﴾

144. Kwa yakini tukiona unavyogeuzageuza uso wako mbinguni. Basi tutakugeuza kwenye Kibla ukipendacho. Basi geuza uso wako upande wa Msikiti Mtakatifu (Al-Kaaba); na po pote mnapokuwa zielekezeni nyuso zenu uliko (msikiti huo); na hakika wale waliopewa Kitabu wanajua kwamba hiyo ni haki itokayo kwa Mola wao; na Mwenyezi Mungu si Mwenye kughafilika na yale wanayoyatenda.

قَدْ نَرَىٰ تَقَلُّبَ وَجْهِكَ فِي السَّمَاءِ ۖ فَلَنُوَلِّيَنَّكَ
قِبْلَةً تَرْضَاهَا ۚ فَوَلِّ وَجْهَكَ شَطْرَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ ۚ
وَحَيْثُ مَا كُنْتُمْ فَوَلُّوا وُجُوهَكُمْ شَطْرَهُ ۗ وَإِنَّ
الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ لَيَعْلَمُونَ أَنَّهُ الْحَقُّ مِنْ
رَبِّهِمْ ۗ وَمَا اللَّهُ بِغَافِلٍ عَمَّا يَعْمَلُونَ ﴿١٤٤﴾

145. Na hao waliopewa Kitabu, hata ukiwaletea hoja za kila namna, hawatafuata Kibla chako; wala wewe hutafuata kibla chao, wala baadhi yao hawatafuata kibla cha wengineo; na kama ukiyafuata matamanio yao baada ya kukufikia ilimu, utakuwa miongoni mwa madhalimu (wenye kudhulumu nafsi zao).

وَلَئِنْ أَتَيْتَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ بِكُلِّ آيَةٍ
مَا تَبِعُوا قِبْلَتَكَ ۚ وَمَا أَنْتَ بِتَابِعٍ قِبْلَتَهُمْ ۚ
وَمَا بَعْضُهُمْ بِتَابِعٍ قِبْلَةَ بَعْضٍ ۚ وَلَئِنِ اتَّبَعْتَ
أَهْوَاءَهُمْ مِنْ بَعْدِ مَا جَاءَكَ مِنَ الْعِلْمِ ۙ
إِنَّكَ إِذًا لَمِنَ الظَّالِمِينَ ﴿١٤٥﴾

---

142. Mtume alipokuwako Makka — anaposali peke yake au pamoja na watu wake — alikuwa akiuelekea ukuta wa kusini wa Al-Kaaba, ili awe kaielekea Al-Kaaba — hiyo iliyoko mbele yake hapo — na iwe kaelekea Baytil Makdis (Baytil Muqaddas) iliyoko Falastin. Aliendelea vivi hivi mpaka alipohama Makka kwenda Madina.

Alipofika Madina — ambayo iko katikati baina ya Makka (kwenye Al-Kaaba) na Baina ya Falastin (kwenye Baytil Muqaddas) ilikuwa haimkiniki kuweza kuvielekea vyote vibla viwili (Al-Kaaba na Baytil Muqaddas) wakati mmoja kama alivyokuwa akiweza alipokuwa Makka.

Basi alikielekea kibla cha Baytil Muqaddas, akakipa mgongo kibla cha Al Kaaba. Alidumu juu ya haya kiasi cha mwaka unusu. Kisha akaambiwa akipe mgongo kibla cha Baytil Muqaddas aelekee cha Al-Kaaba.

Basi hapo ndipo walipotokwa na maneno hao Mayahudi kusema, "Ana nini? Mbona kigeugeu"! Na hali ya kuwa wanaona katika Taurati na Injili kuwa Mtume huyo Muhammad ataelekea huko (Beytil Muqaddas) na huko (Al Kaaba). Wakiyajua haya lakini wakitaka kutukana tu na kuwapoteza watu. Basi Mwenyezi Mungu anamfundisha Mtume Wake jawabu ya kuwajibu.

Masjidul-Aqsa ndio huo Msikiti wa Baitil-Maqdas ambao ulitiwa msingi na Nabii Ibrahim kama alivyoutia msingi Msikiti wa MAKKA (Al-Masjidul-Haraam) na akaujenga. Baada ya kupita miaka 40 tangu kuujenga Msikiti wa Makka ndipo alipoutia msingi Msikiti huu wa Baitul-Maqdis kama ilivyo katika Hadithi ya Mtume Sahihi iliyopokewa na Maimamu hawa:- Muslim, An nassai na Ibnu Maajah.

Kisha ukajengwa vizuri kabisa na Nabii Daud na Nabii Suleiman. Na kusali katika Msikiti huu sala moja ni kama kusali sala hiyo mara elfu katika misikiti mengine, isipokuwa Msikiti wa Madina. Na Imam Al-Bazzar amepokea kuwa kama sala khamsumia.

Na Mtume alisema kama ilivyo katika Hadithi Sahihi iliyopokewa na Maimam wote wa Hadithi kuwa:- "Haifungwi safari kuiyendea Misikiti mengine isipokuwa mitatu hii basi — wa Makka wa Madina na huu wa Baitul-Maqdis.

Na Msikiti huu ulifikwa na maafa mengi — ukavunjwa ukatupwa kabisa kisha ukajengwa tena. Na ilipata kupitiwa na miaka mingi na hali ya kuwa ni kiwanja kitupu.

Kisha katika mwaka wa 17 wa Hijra akautengeza Sayyidna 'Umar Bin Khattab. Basi ukadumu katika mikono ya